



SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

**HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA FEDHA ZA WIZARA YA KILIMO
MALIASILI MIFUGO NA UVUVI**

KWA MWAKA 2019/2020

**ILIYOWASILISHWA NA
MHE. MMANGA MJENGO MJAWIRI (MBM)
WAZIRI WA KILIMO MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI**

MEI, 2019

YALIYOMO

YALIYOMO	i
UTANGULIZI.....	1
UKUAJI NA MCHANGO WA SEKTA YA KILIMO KATIKA PATO LA TAIFA	3
HALI YA UZALISHAJI	4
UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA MWAKA 2018/2019.....	9
MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2018/2019.....	9
MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA MWAKA 2018/2019	12
UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI MWAKA 2018/2019	19
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO	20
Programu Ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji Maji.....	20
Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2018/2019	20
Programu Ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo	22
Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2018/2019	22
Programu Ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo (Chuo Cha Kilimo Kizimbani).....	23
Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2018/2019	23
Programu Ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo.....	25

Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2018/2019	25
Programu ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo.....	28
Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2018/2019	28
Programu Ndogo ya Uhakika wa Chakula Na Lishe.....	30
Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2018/2019	30
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA.....	31
Programu ndogo ya Maendeleo na Uhifadhi wa Misitu.....	32
Utekelezaji wa shabaha kwa mwaka 2018/2019	32
Programu ndogo ya Uhifadhi na Usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka	34
PROGRAMU YA MAENDELEO YA MIFUGO.....	35
Programu Ndogo ya Uzalishaji wa Mifugo.....	36
Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2018/2019	36
Programu Ndogo ya Huduma za Utabibu wa Mifugo	37
Programu Ndogo ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo –ZALIRI.....	38
PROGRAMU YA MAENDELEO YA UVUVI	39
Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvu na Uhifadhi wa Bahari	40
Programu Ndogo ya Ufugaji wa Mazao ya Baharini	41

KAMPUNI YA UVUVI.....	42
Utekelezaji wa Shabaha Kampuni ya Uvuvi ya ZAFICO 2018/2019	42
PROGRAMU YA UTAWALA, MIPANGO NA USIMAMIZI WA KAZI ZA WIZARA.....	44
Programu Ndogo ya Mipango na Usimamizi wa Kazi za Wizara.....	45
Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji.....	47
Programu Ndogo ya Uratibu wa Kazi za Wizara Pemba	49
CHANGAMOTO	49
HATUA ZINAZOCHUKULIWA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO	50
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020.....	51
MAKADIRIO YA MAPATO 2019/2020	51
MAKADIRIO YA MATUMIZI 2019/2020.....	51
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO	55
Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo kwa Mwaka 2019/2020	57
Shabaha Zitakazotolewa na Programu ndogo ya Kilimo Mwaka 2019/2020	59

Shabaha Zitakazotolewa na Wakala wa Serikali na Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo kwa Mwaka 2019/2020	60
Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Uhakika wa Chakula na Lishe kwa Mwaka 2019/2020.....	61
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASLIMALI ZA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA.....	62
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MIFUGO	65
Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Uzalishaji wa Mifugo kwa Mwaka 2019/2020.....	66
Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Huduma za Utabibu wa Mifugo kwa Mwaka 2019/2020.....	66
Programu Ndogo ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo	67
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI.....	68
Programu Ndogo ya Kuimarisha Ufugaji wa Mazao ya Baharini	70
PROGRAMU KUU YA MIPANGO NA UTAWALA WA KAZI ZA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI.....	73
Programu Ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba	77
MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020.....	79
SHUKURANI.....	80
VIAMBATISHO	83

**HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA WIZARA YA KILIMO, MALIASILI,
MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA
2019/2020**

UTANGULIZI

- Mheshimiwa Spika**, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvubi kwa kazi za Kawaida na kazi za Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambayo yanawasilishwa katika mfumo wa Programu (PBB).
- Mheshimiwa Spika**, kwanza kabisa nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuijaalia nchi yetu kuwa na amani, utulivu na kutuwezesha kufikia leo tukiwa wazima na wenyewe afya njema ili tuweze kujadili bajeti hii kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Zanzibar ambapo asilimia kubwa wanajihusisha na kazi za Kilimo, Ufugaji, Uvubi na Uhifadhi wa Maliasili.
- Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuiongoza Zanzibar katika misingi ya umoja, usalama, amani na utulivu. Aidha, tunampongeza Mhe. Rais kwa kusimamia vyema na kupata mafanikio makubwa ya utekelezaji wa malengo ya ILANI ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 – 2020 inayotekelzwa na Serikali ya Mapinduzi

ya Zanzibar katika kufanikisha maendeleo ya Sekta ya Kilimo, kwa lengo la kuongeza tija kwa wananchi na kukuza uchumi. Aidha, tunatoa shukurani za dhati kwa miongozo anayoitoa ambayo imeleta maendeleo na kupiga hatua katika sekta ya kilimo nchini.

4. Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii pia kumshukuru Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuniamini na kunipa nafasi ya kuitumikia Serikali hii; ambapo mnamo tarehe 3/3/2019 ameniteua kuwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Aidha, napenda nichukue fursa hii kumuhakikishia kwamba nipo tayari kutekeleza majukumu yangu na naahidi kwamba nitatumikia Serikali hii kwa uwezo wangu wote kwa kusimamia vyema utekelezaji wa ILANI ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 – 2020 kwa kuleta maendeleo katika sekta ya Kilimo nchini.

5. Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa juhudini zake kubwa za kumsaidia na Kumshauri vizuri Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kutekeleza majukumu yake ya kuiongoza nchi na kuleta manufaa kwa wananchi hasa kwenye Sekta ya Kilimo.

6. Mheshimiwa Spika, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Spika wa Baraza la wawakilishi kwa umakini na umahiri wake

wa kuliendesha Baraza la Wawakilishi, pia nawapongeza Naibu Spika, Wenyeviti na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wanaomsaidia kuliongoza Baraza na tunawaombea dua Mwenyezi Mungu awazidishie uwezo, hekima na busara ili impate wepesi wa kuliendesha baraza kwa ufanisi na mafanikio.

7. Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii adhimu kumshukuru na kumpongeza Mwenyeekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo Mheshimiwa Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini, Mwakilishi wa Jimbo la Dimani na Wajumbe wa Kamati hii kwa miongozo na ushauri wanayoitoa kwa Wizara ya Kilimo katika kufanikisha utekelezaji wa malengo katika bajeti ya Wizara kwa mwaka 2018/2019. Aidha, tunaishukuru Kamati kwa kufanikisha maandalizi ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2019/2020. Napenda kukuhakikishia kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo waliyotupa tume

8. yazingatia na kuyaweka katika bajeti hii ninayoiwasilisha.

UKUAJI NA MCHANGO WA SEKTA YA KILIMO KATIKA PATO LA TAIFA

9. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo inayojumuisha mazao, mifugo, uvuvi, misitu na maliasili zisizorejesheka bado ni tegemeo kubwa kwa uchumi wa Zanzibar na inachangia moja kwa moja kwa wananchi katika kujikimu kimaisha. Sekta ya Kilimo imeajiri takriban asilimia 40 ya wananchi wa Zanzibar na inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wanategemea sekta hii katika kujikimu kimaisha. Lengo kuu la

Wizara ni kuongeza uzalishaji kwa kukutumia mbinu bora na teknolojia za kisasa, utiaji wa thamani, upatikanaji wa masoko na hatimae kukuza viwanda na pato la Taifa sambamba na uhifadhi wa maliasili zetu.

10. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2018, Sekta ya Kilimo imechangia asilimia 21.3 ya Pato la Taifa (mazao asilimia 8.6, mifugo 6.1, maliasili 1.3 na uvuvi 5.2 - OCGS 2018) na kuonesha kushuka ikilinganishwa na asilimia 27.9 mwaka 2017. Kushuka kwa mchango wa Sekta ya Kilimo katika Pato la Taifa kwa mwaka 2018 kumetokana na kutokuwepo kwa mapato ya Uvuvi wa Bahari kuu kwa mwaka 2018 kunatokana na ongezeko la tozo ya TZS 1,100 kwa kilo ya samaki katika leseni ya Uvuvi wa bahari Kuu Tanzania, kupungua kwa mapato yatokanayo na rasilimali zisizorejesheka kutoka TZS 7.3 bilioni mwaka 2017 hadi TZS 4.98 bilioni mwaka 2018. Vilevile upungufu mkubwa uliojitokeza katika uzalishaji wa karafuu kutoka tani 8,277.2 mwaka 2017 hadi tani 675.2 mwaka 2018 na zao la mwani kutoka tani 10,980.89 mwaka 2017 hadi tani 10,424.9 mwaka 2018. Upungufu mazao hayo umetokana na kuwa mwaka 2018 ulikuwa ni msimu mdogo wa uzalishaji wa karafuu na mabadiliko ya tabianchi, yaliyopelekea athari ya maradhi katika zao la mwani.

HALI YA UZALISHAJI

11. Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kwamba jumla ya ekari 95,021.2 zilipandwa mwaka 2018, kati ya hizo ekari

82,506.8 zilipandwa mazao ya chakula (sawa na asilimia 86.8). Kati ya ekari zote zilizopandwa mazao ya chakula, zao la mpunga ndio lilochukua eneo kubwa ambapo ekari 31,186.3 sawa na asilimia 37.8 zilitumika kwa uzalishaji wa mpunga (ekari 29,638.5 mpunga wa kutegemea mvua na ekari 1,547.8 mpunga wa umwagiliaji maji). Zao la pili lililotumia eneo kubwa la uzalishaji ni muhogo ambapo ekari 26,589 zilipandwa ikiwa sawa na asilimia 32.2 ya eneo lote lililopandwa mazao ya chakula na ekari 12,514.4 zilipandwa mazao ya mboga sawa na asilimia 13.2. Eneo dogo la ekari 194.5 sawa na asilimia 0.2 lilitumika kwa upandaji wa mazao ya jamii ya kunde. Aidha, Wizara inatilia mkazo na kuhamasisha wakulima kulima mazao ya jamii ya kunde kwa vile ni chanzo kikuu cha protini itokanayo na mimea.

12. Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha ya kwamba eneo lililopandwa migomba limepungua kutoka ekari 8,517 mwaka 2017 hadi ekari 6,068.4 mwaka 2018, hii ikiwa ni upungufu wa asilimia 28.7. Eneo lililopandwa viazi vitamu limeongezeka kufikia ekari 7,511.5 mwaka 2018 kutoka ekari 4,886 mwaka 2017 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 53.7.

13. Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mazao ya chakula na matunda ulikuwa tani 375,837 mwaka 2018 ikiwa ni ongezeko la asilimia 9 ikilinganishwa na tani 357,932 zilizozalishwa mwaka 2017 (**Kiambatisho nam. 1a**). Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa matunda kwa asilimia 56, viazi vitamu kwa asilimia 54 na mpunga kwa

asilimia 20 ikilinganishwa na uzalishaji wa mwaka 2017. Aidha, kiwango cha uzalishaji kwa eka kwa mazao ya mpunga na viazi vitamu kimeongezeka. Uzalishaji wa mpunga umeongezeka kutoka wastani wa tani 0.9 hadi tani 1.5 kwa eka kwa mpunga wa kutegemea mvua; na kutoka wastani wa tani 2.5 hadi tani 4.5 kwa eka kwa mpunga wa umwagiliaji; na uzalishaji wa viazi vitamu umeongezeka kutoka wastani wa tani 3.2 kwa ekari hadi tani 6. Kwa ujumla ongezeko la uzalishaji wa mazao ya chakula hasa mpunga, mboga na matunda limetokana na hali nzuri ya hewa, mwamko na hamasa ya wakulima kuhusiana na matumizi ya teknolojia ya kisasa ikiwemo kilimo shadidi na kufuata kanuni za kilimo bora ikiwemo kupanda kwa wakati, upatikanaji na matumizi mazuri ya pembejeo ikiwemo mbolea, dawa na mbegu bora.

14. Mheshimiwa Spika, kwa mazao ya mifugo takwimu zinaonesha kuwepo kwa ongezeko la idadi ya Ng'ombe waliochinjwa wanaoletwa kutoka Tanzania Bara 16,874 mwaka 2017 hadi kufikia ng'ombe 20,053 mwaka 2018 sawa na ongezeko la asilimia 48.5. Aidha, kwa upande wa Mbuzi waliochinjwa inaonesha kupungua kutoka Mbuzi 2,739 mwaka 2017 hadi kufikia 2,317 mwaka 2018, ikiwa ni upungufu wa asilimia 15 na Kuku waliochinjwa wamepungua kutoka 819,994 mwaka 2017 hadi kufikia 378,422 sawa na asilimia 52.1. Aidha, kupungua kwa idadi ya Kuku waliochinjwa kumetokana na kuongezeka kwa gharama za chakula cha Kuku kinachotoka nje ya nchi kutoka TZS. 43,000 hadi TZS 60,000 kwa mfuko wa

kilo 50. Vile vile, kuongezeka kwa uingizaji wa kuku na mayai kutoka nje ya nchi pamoja na upatikanaji mgumu wa vifaranga vyta Kuku pia vimechangia katika kupunguza upatikanaji wa kuku na bidhaa zake. Kutokana na tatizo hilo Wizara tayari imekamilisha utafiti wa viwango sahihi vyta chakula cha kuku na inakamilisha utaratibu wa manunuvi wa mtambo wa kutengenezea chakula cha kuku kwa ajili ya kutatua tatizo hili.

15. Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa samaki umeongezeka kutoka tani 35,057.2 mwaka 2017 hadi kufikia tani 35,441 mwaka 2018 sawa na asilimia moja ya ongezeko hilo, Mazao ya baharini yaliyosafirishwa yameongezeka kutoka tani 40.49 mwaka 2017 hadi tani 102.48 mwaka 2018 ikiwemo Majongoo, Kaa na Pweza (**Kiambatisho nam. 1b**). Pamoja na kuongezeka uzalishaji wa samaki bado hatujafikia mahitaji ya tani 44,400 za samaki kukiwa na upungufu wa tani 8,959 ambazo zinahitajika kukidhi mahitaji ya ndani na soko la uthali nchini (watalii 522,000) kwa mwaka 2018. Wizara inaendelea na juhudi za kushajiisha wananchi katika ufugaji wa mazao ya baharini, upatikanaji wa vifaranga pamoja na kuwashajiisha wavuvi kuvua katika kina kirefu cha maji.

16. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uhifadhi wa misitu na maliasili zisizorejesheka, takwimu zinaonesha kwamba matumizi ya boriti yamepungua kwa asilimia 5.3 (2,244.1 mita za ujazo) ikilinganishwa na mwaka 2017. Matumizi ya fito kwa ajili ya ujenzi yameongezeka kwa asilimia 34.3 kutoka mita za ujazo 3,304 mwaka 2017 hadi 4,438 mwaka 2018. Aidha,

matumizi ya nishati ya kuni yameongezeka kutoka mita za ujazo 23,114 mwaka 2017 hadi mita za ujazo 26,569 mwaka 2018 sawa na asilimia 14.9 ya ongezeko la matumizi (**Kiambatisho nam. 1c**). Wizara inaendelea kushajiisha wananchi matumizi ya gesi salama na majiko sanifu kwa ajili ya kupunguza matumizi ya nishati ya kuni na kuhamasisha upandaji wa miti kwa ajili ya ujenzi.

17. Mheshimiwa Spika, uchimbaji na matumizi ya mawe umeongezeka kutoka tani 91,728 mwaka 2017 hadi tani 132,434 mwaka 2018 sawa na asilimia 44.4; matumizi ya kifusi yameongezeka kutoka tani 58,541 mwaka 2017 hadi tani 65,985 mwaka 2018 sawa na asilimia 113 na mchanga kutoka tani 832,043 mwaka 2017 hadi kufikia tani 948,329 mwaka 2018 sawa na asilimia 144.4 (**Kiambatisho nam. 1d**). Ongezeko la matumizi ya rasilimali zisizorejesheka limetokana na kasi kubwa ya ujenzi wa miradi ya maendeleo ikiwemo barabara, mahoteli, nyumba za makaazi, nyumba za ibada, Maskuli na majengo kwa ajili ya makaazi kwa watumishi wa Serikali na Maofisi. Wizara inaendelea kuchukua juhudzi za udhibiti wa matumizi ya rasilimali zisizorejesheka kwa kuwaelimisha wananchi juu ya matumizi mbadala ya malighafi za ujenzi na kuweka utaratibu mzuri ili kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali zetu.

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2018/2019

18. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/19, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvu imesimamia utekelezaji wa malengo ya Dira ya 2020, ILANI ya Uchaguzi ya CCM 2015 – 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA III), Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), Mipango Mikakati ya Kisekta pamoja na Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Kilimo (ATI). Utekelezaji wa Mikakati na Malengo hayo kumepelekea kuongezeka kwa taaluma na teknolojia kwa wakulima, wafugaji na wavuvi jambo ambalo limeongeza ari na hamasa na hatimae kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na kuwa na uhakika wa chakula na lishe bora nchini.

MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2018/2019

19. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara ilikadiriwa kukusanya **TZS 12.5 bilioni** kutokana na vyanzo vyake 12 vya mapato. Kwa kipindi cha Julai hadi April, 2019 imekusanya jumla ya **TZS 5.85 bilioni** sawa na asilimia **56.0** ya makadirio. (**Kiambatisho nam.2**). Kushuka kwa mapato kumechangiwa na kukosekana kwa mapato yatokanayo na leseni za uvuvu wa baharí kuu, ukodishaji wa mashamba ya karafuu na uzalishaji wa zao la mwani.

20. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2018/19 Wizara ilikadiriwa kutumia jumla ya **TZS 62.62 bilioni** kati ya fedha hizo **TZS 23.23 bilioni** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS 14.45 bilioni Mishahara, TZS 5.66 bilioni matumizi mengineyo na TZS 3.13 bilioni ikiwa ni Ruzuku kwa ajili ya Chuo cha Kilimo Kizimbani, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo na **TZS 39.38** kwa ajili ya miradi ya maendeleo kati ya hizo **TZS 33.73 bilioni** kutoka kwa washirika wa maendeleo na **TZS 5.65 bilioni** ni mchango kutoka SMZ.

21. Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha Julai 2018 hadi Aprili, 2019, Wizara imepatiwa jumla ya **TZS 67.20 bilioni** sawa na asilimia 108 ya fedha zilizoombwa. Kati ya fedha hizo **TZS 19.66** kwa ajili ya kazi za kawaida ambapo TZS 11.66 bilioni mishahara; TZS 5.40 bilioni kwa matumizi mengineyo na TZS 2.59 bilioni kwa Ruzuku za Chuo cha Kilimo Kizimbani, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo (**Kiambatisho nam. 3**). Aidha, Wizara imepata **TZS 47.55 bilioni** kwa kazi za miradi ya maendeleo (TZS 46.07 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo na TZS 1.48 bilioni kutoka SMZ) (**Kiambatisho nam. 4**). Ongezeko la upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo limetokana na kuanza kwa utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Maji kupitia mkopo kutoka EXIM BANK ya Korea.

22. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ilitekeleza malengo yake kupitia programu zake kuu tano ambazo ni:

- a) Programu ya Maendeleo ya Kilimo;
- b) Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu na Maliasili Zisizorejesheka;
- c) Programu ya Maendeleo ya Mifugo;
- d) Programu ya Maendeleo ya Uvuvi; na
- e) Programu ya Mipango na Utawala wa Kazi za Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

23. Aidha, Wizara iliendelea na kusimamia utekelezaji wa miradi na Programu 10 za maendeleo ikiwemo Mradi wa kuendeleza miundombinu ya masoko na fedha vijijini - MIVARF, Mradi wa usimamizi wa kazi za uvuvi wa kanda ya kusini mashariki mwa bahari ya Hindi - SWIOFish, Mradi wa kuendeleza uzalishaji wa zao la mpunga - ERPP, Mradi wa kuwaunganisha wakulima na wazalishaji wa mazao ya mboga - Agri-Connect, Mradi wa udhibiti wa sumukuvu katika mazao ya nafaka- TANIPAC, Mradi wa kukabiliana na kilimo cha mabadiliko ya hali ya hewa - Climate Smart Agriculture, Mradi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji, Mradi wa kuendeleza miundombinu ya sekta ya kilimo, Mradi wa

kutotolea vifaranga vya samaki na Mradi wa usimamizi wa matumizi ya misitu ya mwambao.

MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA MWAKA 2018/2019

24. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imepata mafanikio yafuatayo:

- a) Kuongezeka kwa uzalishaji wa mpunga kutoka tani 39,683 mwaka 2017 hadi kufikia tani 47,507 mwaka 2018 ambazo ni sawa na tani 31,273 za mchele (asilimia 39) ya mahitaji yetu ya tani 80,000 kwa mwaka;
- b) Kwa msimu wa mwaka 2018/2019 Wizara imehamasisha uzalishaji wa miche mbalimbali. Jumla ya miche 4,520,850 imeoteshwana katika vitalu vya Serikali na watu binafsi Unguja na Pemba. Aidha, miche 1,128,639 imeoteshwana Wizara (Unguja 932,674 na Pemba 195,965) ikiwemo Mikarafuu 304,660, matunda na viungo 156,516, minazi 86,631na misitu 580,832. Aidha, Wizara ilihamasisha wazalishaji wenye vitalu binafsi ambapo wameweza kuzalisha jumla ya miche ambapo
- c) Wizara kwa kushirikiana na taasisi ya TAHA tayari imeanza utekelezaji wa programu ya kuwaunganisha vijana 40 katika Kilimo cha Vanila, Pilipili hoho, Manjano, Tangawizi na Pilipili Manga katika maeneo ya mashamba ya mipira na shamba la Bungi yenye ukubwa wa hekta tano kwa msimu huu wa mvua

za masika 2019. Vilevile, vijana 50 Wakizanzibari waliomaliza mafunzo ya JKT wamepatiwa eneo la ekari tano (5) Kizimbani kwa ajili ya kuendeleza mazao ya mboga;

d) Kukamilika kwa Ghala la akiba ya chakula lenye uwezo wa kuhifadhi tani 500 za mchele na vifaa vyenye thamani ya milioni 78 vimenunuliwa.

e) Matrekta 33 (Unguja 23 na Pemba 10) yalitoa huduma ya uchimbaji na uburugaji wa mashamba ya wakulima ekari 27,258 Unguja na Pemba ikilinganishwa na lengo la ekari 21,000. Aidha, jumla ya ekari 22,219 (6,729.75 Unguja na 15,489.55 Pemba) zimeshapandwa;

f) Jumla ya tani 650 za mbolea, tani 200 za mbegu ya mpunga na lita 7,211 za dawa ya kuulia magugu zimenunuliwa na zinaendelea kusambazwa kwa wakulima kupitia mpango wa ruzuku; Wizara pia, kupitia Mradi wa ERPP imenunua na kusambaza tani za mbolea 65.9 (UREA tani 53.9, DAP tani 4 na TSP tani 8) katika mabonde ya umwagiliaji yaliyo chini ya Mpango wa Ruzuku wa Mradi wa ERPP;

g) Wizara imeanzisha na kuzindua kampeni ya kuendeleza zao la nazi nchini ambapo jumla ya Miche 86,631 (Unguja 61,631 na Pemba 25,000) ya minazi imeoteshwa na inaendelea kusambazwa kwa wananchi bila ya malipo. Aidha, Wizara imeanzisha mashamba mawili ya mbegu za minazi yenye ukubwa wa hekta 9.3 (5.3 Selem Unguja na 4.0 Tumbe Pemba). Vilevile Wizara imekamilisha matayarisho ya Sera ya Minazi na

imo katika hatua za mwisho za utayarishaji wa Sheria ya kuendeleza Minazi nchini.

h) Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Chuo cha Taifa SUZA imekamilisha hatua za awali za kuunganisha chuo cha Kilimo Kizimbani kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Taifa. Aidha, Serikali imeshapata mtaala kutoka chuo cha Kilimo cha Sokoine na Shahada ya kwanza ya Kilimo mjumuisho inatarajiwa kuanzishwa katika muhula wa masomo wa Oktoba 2019. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa hivi sasa inakamilisha hatua za uwekaji wa miundombinu na kutayarisha walimu wa kufundisha.

i) Vikundi viwili (Kilimo Mkombozi cha Mkokotoni na Wakulima SACCOS cha Bumbwisudi) vimekamilisha taratibu zote za kupatiwa mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo ya Tanzania – TADB. Vikundi hivi vitapatiwa Matrekta mawili na zana zake yenye thamani ya TZS 160,020,000;

j) Wanyama 53,543 walichanjwa dhidi ya maradhi mbali mbali ya mifugo na ng'ombe 1,784 walipandishwa kwa sindano (Unguja 1,124 na Pemba 660). Hii imesaidia kupunguza kasi ya maambukizi ya maradhi katika mifugo pamoja na kuongeza idadi ya ng'ombe wa maziwa;

k) Wizara imekamilisha tafiti mbili za tathmini ya uzito na ubora wa nyama ya ng'ombe na tathmini ya uzito wa kuku wanaotumia chakula cha madukani na kilichotengenezwa na taasisi ya utafiti. Matokeo ya utafiti yameonesha kwamba

viwango nya uzito wa ng'ombe wa aina ya ZEBU ni mdogo kulinganisha na wa Tanzania Bara ambapo wastani wa ng'ombe wetu ni kilo 146 kabla ya kuchinjwa na asilimia 48 ya uzito ni nyama;

- l) Watalii 38,371 wa ndani (Unguja 7,851 na Pemba 2,132) na wa nje (Unguja 28,240 na Pemba 148) walitembelea katika hifadhi za Kiwengwa, Masingini, Jozani na Ngezi.
- m) Doria 169 (Unguja 124 na Pemba 45) zimefanyika na kufanikiwa kukamata na kuchoma moto misumeno ya moto 346 (Unguja 206 na Pemba 140), gari 15 za mizigo na gari 15 za ng'ombe.
- n) Doria shirikishi 174 katika maeneo ya hifadhi za bahari zilifanyika. Matokeo ya doria yamebainisha kwamba wavuvi 3,839 hawakuwa na leseni na kulazimika kukata leseni zenye thamani ya TZS 5,758,500;
- o) Mafunzo ya upandaji mwani katika kina kirefu cha maji yalifanyika katika vijiji 48 (Unguja 15 na Pemba 33). Aidha, kamati 81 za wakulima wa mwani zilipatiwa vifaa nya kulimia ikiwemo kamba/roli 1,222 na taitai 2,250.
- p) Kufuatia ziara ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein nchini Indonesia iliyofanyika mwezi wa Agosti, 2018 Wizara inaendelea na utafiti wa mwani aina ya “**Agar Glacelaria**” wenye thamani kubwa na utakaongeza tija kwa

wakulima ukilinganishwa na tulionao hivi sasa. Aidha, kutokana na ziara hiyo “MOU” mbili (2) zimetayarishwa kwa ajili ya mashirikiano katika sekta ya Kilimo na Uvuvi amabzo zitasainiwa hivi karibuni. Vilevile, Taasisi ya utafiti wa Kilimo Zanzibar inaendelea kushirikiana na Taasisi za Utafiti za Indonesia kuhusu Maendeleo ya Kilimo cha Minazi nchini.

q) Vifaranga 240,000 vya majongoo baharí vimezalishwa kupitia kituo cha kutotolea vifaranga vya samaki kilichopo Beit-el-Ras kati ya hivyo majongoo baharini 9,000 vimesambazwa katika mashamba ya mfano yaliopo Uzi. Vifaranga vya kaa 2,000,000 vimezalishwa na vinatarajia kusambazwa kwa wakulima katika mashamba ya mfano. Aidha, vikundi 158 (Unguja 72 Pemba 86) vya wafugaji wa majongoo wamepatiwa mafunzo ya mbinu bora za ufugaji wa mazao ya baharini ikiwemo samaki, majongoo na mwani.

r) Wizara ipo katika hatua za mwisho za utengenezaji wa boti ya Uvuvi nchini Srilanka kupitia Kampuni ya ZAFICO na inatarajiwu kufika mwisho wa mwezi wa Aprili 2019. Wizara imekamilisha utaratibu wa manunuza wa boti ya pili ya Uvuvi kutoka nchini Maldives. Aidha, mtambo wa kutengeneza barafu katika soko la Tumbe – Pemba umeanza kazi kuanzia Machi, 2019.

s) Wizara imesaini mkataba wa Ujenzi wa Miundombinu ya Kilimo cha Mpunga wa Umwagiliaji maji wenye thamani ya Dola za Kimarekani Milioni 59.9 wenye ukubwa wa jumla ya

hekta 1,524 katika mabonde ya Cheju, Kilombero, Kibokwa, Kinyasini, Mlemele na Makwararani. Aidha, Mkandarasi yupo katika hatua za kuajiri wafanyakazi, uletaji wa vifaa kwa ajili ya ujenzi.

- t) Wizara kwa kushirikiana na taasisi za Umma na Serikali zimefanikisha maonesho ya Kilimo (Nane Nane) huko Dole na maonesho ya siku ya chakula Duniani yalifanyika huko Chamanangwe Wilaya ya Wete Pemba. Jumla ya taasisi 104 za Serikali na watu binafsi zilishiriki katika maonesho ya Kilimo na taasisi 86 zilishiriki maonesho ya siku ya Chakula Duniani ambayo kiujumla yalifana sana. Kufanyika kwa maonesho haya kumeongeza hamasa na muamko kwa wananchi katika sekta ya kilimo na kushajiika katika matumizi ya teknolojia na huduma zinazotolewa.
- u) Kuanzishwa kwa taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini, hatua hii itasaidia katika kuleta ufanisi na kutatua changamoto zilizopo katika sekta ya uvuvi;
- v) Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na taasisi nyengine hapa Zanzibar imekamilisha matayarisho ya programu ya sekta ya Kilimo yenye lengo la kuleta maendeleo na mageuzi katika Sekta ya Kilimo Zanzibar kukifanya kilimo kuwa cha kisasa, jumuishi na chenye ushindani ili kuchochaea sekta za viwanda na utalii, kuleta tija na hali bora za maisha kwa kutumia dhana ya mnyororo wa thamani.

- w) Wizara kwa kushirikiana na Shirika la ICIPE la nchini Kenya inaendelea kutoa elimu kwa jamii kwa kutumia njia shirikishi katika kuangamiza nzi wa matunda. Wizara imepokea mitego 2,080 kutoka shirika hilo kwa ajili ya kuangamiza wadudu wa matunda, mitego hio imesambazwa Unguja na Pemba. Vilevile, Wizara kwa kupitia Shirika la Nguvu za ATOMIC imekamilisha andiko la mradi wa kuangamizi nzi wa matunda, mradi huo hivi sasa unafanyiwa mapitio na unategemea kuanza mwaka 2020.
- x) Wizara imekamilisha taratibu za kumpata mkandarasi (MASIM COMPANY) kwa ajili ya ujenzi wa Uzio wa kituo cha Karantini cha Gando Nzi wengi Pemba. Aidha, Wizara pia imekamilisha ulipaji wa fidia wa TZS 138,066,500 kwa wanakijiji 40 waliozunguka eneo hilo la kituo cha karantine ya mifugo cha Gando Pemba.
- y) Malipo ya fidia TZS 863,083,800 kwa wananchi 2,059 (633 Unguja na 1,426 Pemba) katika utekelezaji wa miradi ya MIVARF, ERPP, Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya umwagiliaji maji na Malipo ya kifuta jasho cha TZS 391,082,500 kwa wananchi 816 waliopo Pemba wanaoyatunza mashamba ya mikarafuu;
- z) Kusainiwa kwa mkataba na kampuni ya Rinkai Nissan Construction Company ya Japan kwa ajili ya ujenzi wa soko la kisasa la samaki Malindi. Aidha, ujenzi huu unatarajiwa kuanza hivi karibuni;

- aa) Wizara tayari imeajiri watendaji 55 Pemba na imekamilisha usaili wa vijana 78 kwa upande wa Unguja. Vile vile imetoe tangazo kwa ajili ya kujaza nafasi tupu 114;
- bb) Jumla ya wanafunzi 194 (AStashahada 84 na Stashahada 110) walihitimu mafunzo yao katika mahafali ya mwaka 2018;
- cc) Jumla ya mabanda manne (4) ya kisasa ya kufugia nyuki yamejengwa maeneo ya Kiwengwa, Jambiani, Mtende kwa Unguja na Tovuni kwa Pemba kwa ajili ya kuwaunganisha vijana na kuwapatia ajira;
- dd) Watendaji 5 katika ngazi ya shahada ya Uzamivu (PhD) tayari wamerudi masomoni na wameshapangwa kazi (1 Wizara 4 Taasisi ya Utafiti wa Kilimo). Aidha, watendaji 13 (3 Phd na 10 MSc) kupitia Mradi wa SWIOFish tayari wapo masomoni. Wafanyakazi watatu wanaendelea na masomo PhD nchini China (2) na Misri (1). Pia vijana 37 wanaendelea na mafunzo ya utibabu wa wanyama nchini China katika ngazi ya Shahada ya kwanza.

UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI MWAKA 2018/2019

25. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa shabaha za Wizara ya Kilimo kupitia Programu zake kuu tano (5) na ndogo 13 ulikuwa kama ifuatavyo:

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO

26. Mheshimiwa Spika, Programu Kuu ya Maendeleo ya Kilimo inajumuisha programu ndogo nne; Programu Ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji Maji, Programu ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo, Programu ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo, Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na zana za Kilimo na Programu Ndogo ya Uhakika wa Chakula na Lishe.

Programu Ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji Maji

27. Mheshimiwa Spika, Programu hii inatekelezwa kupitia Idara ya Umwagiliaji Maji na ina jukumu la kuendeleza na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji nchini, kwa kutoa taaluma za uzalishaji na kiufundi juu ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu, kushajiisha na kusimamia jumuiya za wakulima kwenye mabonde ya umwagiliaji maji.

Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2018/2019

- a) Ujenzi wa mitaro kwa kiwango cha saruji katika mabonde ya Mtwango (mita 3,000) umekamilika na Kwale Mpona (mita 1500) unaendelea. Ujenzi huu unatekelezwa kupitia Mradi wa ERPP.
- b) Uungaji umeme (High tension) umefanyika katika mabonde ya Mchangani Mayungi, Kibonde Mzungu, Koani, Bandamaji kwa Unguja na Dobi na Ole kwa Pemba kupitia mradi wa ERPP). Aidha, kazi za uungaji umeme katika bonde la Machigini zimekamilika.

- c) Ununuzi na uingizaji wa pampu katika kisima kipyka kilichopo eneo la PADEP lililopo bonde la umwagiliaji la Cheju pamoja na uchimbaji wa kisima Machekechuni kwa ajili ya kuwaendeleza wakulima wa mboga;
- d) Usimamizi wa uchimbaji wa visima sita vipyta katika mabonde ya Kibonde Mzungu, Bandamaji, Koani, Dobi, Ole na Machigini umefanyika kupitia mradi wa ERPP.
- e) Wakulima 28 katika bonde la Chaani wamelipwa fidia kwa mazao yatakayoathirika wakati wa ujenzi wa miundombinu ambapo jumla ya TZS 45.96 milioni zimeshalipwa.

28. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 programu ndogo hii iliombewa jumla ya **TZS 10.11 bilioni** ambapo (**TZS 7.11 Mshahara**, **TZS 400.00 milioni** kwa matumizi mengineyo, **TZS 500.00 milioni** fedha za maendeleo kutoka SMZ na **TZS 8.5 bilioni** kutoka kwa washirika wa maendeleo EXIM BANK). Hadi kufikia Aprili, 2019 programu imepata **TZS 43.71 bilioni** sawa na asilimia 433 ya fedha zilizoombwa. Kati ya fedha hizo **TZS 577.97 milioni** mishahara; **TZS 368.9 milioni** kwa matumizi mengineyo. Aidha, **TZS 500.00 milioni** fedha za maendeleo kutoka SMZ na **TZS 42.26 bilioni** kutoka kwa washirika wa maendeleo EXIM BANK ya Korea.

Programu Ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo

29. Mheshimiwa Spika, Programu hii inatekelezwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Chuo cha Kilimo Kizimbani, lengo ni kuimarisha na kuendeleza Tafiti za Kilimo na Maliasili pamoja na kuimarisha uwezo wa Chuo cha Kilimo Kizimbani katika kuongeza wataalamu wa fani ya Kilimo na Mifugo.

Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2018/2019

30. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019, programu imetekeliza shabaha zifuatazo:

- a) Tafiti mbili (2) za mpunga kuangalia ustahamilivu wa mbegu za mpunga dhidi ya maradhi ya ukungu kwa kutumia mbinu za mionzi; na tafiti ya kutathmini ubora wa mbegu za mpunga za kigeni katika mazingira ya Zanzibar zimefanyika na zinaendelea.
- b) Tafiti ya kuangalia athari ya mchanganyo wa mazao ya mihogo na viazi (intercropping) katika uzalishaji zimefanyika na zinaendelea.
- c) Tafiti mbili za mboga kuangalia athari ya kukata vilele katika uzalishaji na ubora wa matikiti maji na matumizi ya mbolea za asili katika uzalishaji wa pilipili boga zimefanyika.
- d) Tafiti 4 zimeanzishwa Unguja kwa mazao ya mpunga, migomba, kunde na 1 mazao ya mboga) na tafiti 2 za muhogo na sunflower zimeanzishwa kwa upande wa Pemba;

- e) Matayarisho ya ununuzi wa vifaa vyaa ujenzi wa ofisi unaendelea. Aidha, kazi ya ujenzi wa uzio wa mita 55 unaendelea
- f) Kikao cha Kwanza cha Baraza kiliitishwa na kilipokea ripoti ya utekelezaji.

31. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar iliombewa jumla ya **TZS 2.24 bilioni** (TZS 1.92 bilioni Mshahara na 315.00 milioni kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Aprili, 2019 taasisi imepata **TZS 1.82 bilioni** (TZS 1.56 bilioni mishahara na TZS 268.46 milioni kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 82 ya fedha zilizoombwa.

Programu Ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo (Chuo Cha Kilimo Kizimbani)

32. Mheshimiwa Spika, programu hii inatekelezwa na Chuo cha Kilimo Kizimbani na kina jukumu la kutoa mafunzo katika fani za kilimo, maliasili na mifugo katika ngazi tofauti. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, program imetekeliza shabaha zifuatazo:

Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2018/2019

- a) Wanafunzi 293, Stashahada 75 na Astashahada 218 (kilimo 168 na mifugo 125) wamefundishwa na kufanya mitihani ya Muhula wa Kwanza;

- b) Kikao baina ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na SUZA kilifanyika tarehe 16 Julai, 2018. Wajumbe walikubaliana kuwa SUZA wataongoza utekelezaji wa kukamilisha utaratibu wa Chuo kijiungu na SUZA na kuanzisha Shahada ya Kilimo Mjumuisho mwaka wa masomo 2019;
- c) Mazungumzo kuhusu kulipima eneo la RAZABA baina ya Wizara ya Kilimo na Shirika la Taifa la Nyumba Tanzania Bara yamekamilika na MoU tayari imeridhiwa na Mwanasheria wa Serikali ya Mapinduzi, Zanzibar.
- d) Wakulima 80 wa Bonde la Maotwe Kangani, Pemba wamefundishwa kilimo bora cha mpunga wa umwagiliaji maji.
- e) Muundo wa Utumishi wa Taasisi uliwasilishwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma na kupokelewa. Kabla ya kujadiliwa, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar imetakiwa kutayarisha muhutasari wa muundo huo na kuwasilisha Kamisheni ya Utumishi wa Umma kwa ajili ya Kuzingatiwa.

33. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Programu iliombewa **TZS 928.00** milioni ikiwa ni Ruzuku kwa kazi za kawaida (TZS 812.70 milioni Mishahara na TZS 115.30 milioni matumizi mengineyo). Hadi kufikia Aprili, 2019 Chuo kimepata **TZS 765.01** milioni (TZS 652.25 milioni mishahara na TZS 112.83 milioni kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 83 ya fedha zilizoombwa.

Programu Ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo

34. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo inatekelezwa kuititia Idara ya Kilimo ina majukumu ya kusimamia maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, kutoa elimu ya uzalishaji na ushauri wa kitaalam kwa wakulima.

Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2018/2019

35. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, program kuititia Idara imetekeliza yafuatayo:

- a) Tani 185 za mbegu ya mpunga, lita 7,211 za dawa ya magugu na tani 650 za mbolea zimenunuliwa na kusambazwa kwa wakulima.
 - b) Ekari 3 za mahindi na ekari 1 ya mtama zimepandwa shamba la Bambi msimu wa masika 2019 kwa ajili uzalishaji mbegu. Aidha, ekari 3 za alizeti zimepandwa kwa ajili ya maonesho na mafunzo kwa wakulima.
 - c) **Uendelezaji wa zao la alizeti;** wakulima 100 (74 wanaume, 26 wanawake) wamepatiwa mafunzo ya uzalishaji, uhifadhi, matumizi na ukamuaji wa mafuta ya alizeti.
- Wataalamu 4 wamefanya ziara ya kimafunzo Morogoro kujifunza kwa vitendo mnyororo mzima wa zao la alizeti, kuanzia shambani hadi sokoni kwa kushirikiana na Taasisi ya Udhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI).

- Shamba la mbegu za alizeti lilianzishwa Pemba ambapo tani 0.5 za mbegu ya aina ya “record” zimezalishwa katika kituo cha Dodeani. Mbegu hiyo itagaiwa kwa wakulima katika msimu wa Masika 2019. Aidha, mashamba 4 ya mafunzo (moja katika kila Wilaya) kwa mashirikiano na mabwanashamba wa Mabaraza ya Miji ya Wete (Mchangamdogo), Chake (Vitongoji), Mkoani (Mtangani) na Halmashauri ya Micheweni (Mtemani-Wingwi).
 - Tani 0.6 za mbegu ya alizeti zimegawiwa kwa wakulima katika msimu wa Masika 2018 katika kisiwa cha Unguja. Jumla ya kilo 2,902 za mbegu za alizeti kutoka kwa wakulima (Pemba kilo 1111.5 na Unguja kilo 1,790.5) zimekamuliwa mafuta lita 892 (Pemba lita 312 na Unguja lita 580) yenye thamani ya Tshs. 3,570,000 katika viwanda vya ukamuaji mafuta ya alizeti Bambi na Ole Dodeani. Wakulima wachache walilima alizeti katika mwaka uliopita kutokana na kuwepo kwa mvua ambazo zilikua juu ya kiwango kwa zao la alizeti).
- d) **Uendelezaji wa mazao ya viungo;** jumla ya eka 6 za manjano, tangawizi, Iliki na vanilla zimepandwa na vikundi 12 vya vijana kwenye mashamba ya mipira ya Maziwani (3), Sanaa (1), Pogwa (1), na Finya (6) katika Wilaya ya Wete, Pemba. Kila kikundi kimepatiwa mbegu za eneo la nusu eka na sasa wanaendelea na upanuzi wa maeneo hayo. Katika kisiwa cha Unguja jumla ya ekari sita (6) zimepandwa manjano, tangawizi, Iliki, vanilla mdalasini na pilipili hoho

shamba la Bungi, Wilaya ya Kati na Kichwele, Wilaya ya Kaskazini “B”, Unguja. Mashamba haya yanatumia teknologia ya umwagiliaji maji kwa njia ya matone. Vikundi vinne vya vijana vyenye washiriki 40 vinahusika katika uanzishaji wa mpango huu. Moja ya kikundi hicho kinahusisha vijana waliomaliza mafunzo katika Chuo cha Kilimo Kizimbani. Mpango huu wa ajira kwa vikundi vya vijana unatekelezwa kwa kushirikiana na Jumuiya ya TAHA na Halamashauri za Wilaya husika.

- e) **Udhibiti wa Nzi wa matunda kwa njia mchanganyiko IPM;** mafunzo ya mwezi mmoja juu ya udhibiti wa viumbe waharibifu wa mboga na matunda kwa njia mchanganyiko yametolewa na wataalamu wa Kichina. Wahusika walikuwa ni 52 wakiwemo wataalam wa Wizara ya Kilimo na JKU, mabwana/mabibi shamba na wakulima.
- f) Kwa kushirikiana na Mabaraza ya Manispaa na Hal mashauri za Wilaya wakulima katika maeneo ya mfano wamepatiwa elimu juu ya uzalishaji bora wa mpunga katika mabonde yote ya mpango.
- g) Tani 4.6 za mbegu za viazi lishe zimegawiwa kwa wakulima 130 ambaao walizigawa kwa wakulima wenzao. Aidha, ekari 1.5 (Unguja 0.75 na Pemba 0.75) imeoteshwa mbegu za viazi lishe na mihogo kwa ajili ya kuzigawa kwa wakulima.
- h) Tani 212.89 za karafuu kavu, tani 6.50 za makonyo na tani 73,307.57 za mazao ya kilimo kutoka na kwenda Tanzania

Bara na nje ya nchi zilikaguliwa katika vituo vya ukaguzi kwa lengo la kudhibiti maradhi na wadudu waharibifu wa mazao.

36. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Programu iliombewa. **TZS 3.68 bilioni** kwa kazi za kawaida (TZS 1.70 bilioni ni Mishahara na TZS 1.98 bilioni matumizi mengineyo). Hadi kufikia Aprili, 2019 programu imepata **TZS 3.44 bilioni** (TZS 1.45 bilioni mishahara na TZS 1.99 bilioni kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 94 ya fedha zilizoombwa.

Programu ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo

37. Mheshimiwa Spika, Programu hii inatekelezwa kupitia Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ambapo ina jukumu la kutoa huduma za matrekta kwa wakulima, sekta binafsi, Taasisi na kuhamasisha matumizi mazuri ya matrekta na zana za kilimo.

Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2018/2019

- a) Matrekta 33 (Unguja 23 na Pemba 10) yalitoa huduma ya uchimbaji na uburugaji wa mashamba ya wakulima.
- b) Matrekta 47 yaliyopo Karakana Kuu na ya mashambani Unguja na Pemba yamekaguliwa kwa kina na kufanyiwa tathmini ya mahitaji ya vifaa. Jumla ya matrekta 26

yalifanyiwa matengenezo na majembe 26 ya kuchimbulia na 10 ya kuburugia.

- c) Matrekta 33, majembe 26 ya kulimia na majembe 10 ya kuburugia yametengenezwa na kupelekwa mashambani kwa ajili ya kutoa huduma za matrekta;
- d) Vipuri vyatya matrekta vyenye thamani ya TZS 455,000,000 vimenunuliwa kupitia Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo. Aidha, matrekta matatu mapya (2 Unguja na 1 Pemba) na Powertiller sita (3 Unguja na 3 Pemba 6) za msaada zimepokelewa kutoka Ubalozi wa Kuwait;
- e) Mafunzo ya nadharia kwa madereva, mafundi na wahandisi wasaidizi yalifanyika Karakana ya Mbweni, na mafunzo ya vitendo yalifanyika Kizimbani upande wa Unguja. Na mafunzo ya nadharia kwa upande wa Pemba yalifanyika Karakana ya Wawi na yale ya vitendo yalifanyika Vitongoji (shambani). Jumla ya washiriki 35 kwa Unguja na 25 kwa Pemba walishiriki mafunzo hayo yaliyoendeshwa na wataalamu kutoka Kampuni za MAHINDRA & MAHINDRA na NEW HOLLAND.

38. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Programu ndogo hii iliombewa jumla ya **TZS 1.37 bilioni** ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini (TZS 644.70 milioni ni mshahara na TZS 725.00 milioni kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Aprili, 2019 Wakala imepata **TZS 1.25 bilioni** (TZS 524.12

milioni mshahara na TZS 723.93 milioni kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 92 ya fedha zilizoombwa.

Programu Ndogo ya Uhakika wa Chakula Na Lishe

39. Mheshimiwa Spika, programu hii inatekelezwa na Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe kwa lengo la kuratibu upatikanaji wa chakula na lishe bora nchini na kufuutilia na kutathmini hali ya uhakika wa chakula na lishe kwa makundi mbali mbali ya wananchi.

Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2018/2019

40. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, program kuititia Idara imetekeliza yafuatayo:

- a) Idara imeazimisha siku ya Afya ya Jamii (Community Health Day) katika Shehia 10 (5 Unguja na 5 Pemba).
- b) Ufuutiliaji na Tathmini ya mradi wa ufugaji wa kuku wa kienyeji na mboga umefanyika katika Wilaya ya Kaskazini ‘A’ Micheweni na Chake chake.
- c) Ufuutiliaji wa hali ya chakula nchini umefanyika ambapo takwimu na taarifa zimekusanya na kufanyiwa uchambuzi. Aidha, ripoti ya Hali ya Chakula Zanzibar kwa mwaka 2018 imetayarishwa na kusambazwa kwa wadau;
- d) Wafanyakazi wanne wa Idara wamepatiwa mafunzo juu ya utayarishaji wa Muongozo wa Matumizi ya Chakula (Food-based Dietary Guideline). Mafunzo haya yametolewa na

Wataalam kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo (SUA) na yanafadhiliwa na FAO. Aidha, Idara hivi sasa chini ya msaada wa kitaalamu unaotolewa na Wataalam kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo (SUA) inashirikiana na watendaji kutoka kitengo cha Lishe Wizara ya Afya, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Biashara, Kitivo cha Afya cha Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA), Wakala wa Chakula dawa na Vipodozi katika utayarishaji wa Muongozo wa Matumizi ya Chakula.

- e) Watumishi wanne (4) wa Idara wamepatiwa mafunzo yanayohusu Uchambuzi wa Hali ya Chakula Nchini (Food Balance Sheets) mafunzo haya yalitolewa na Mtaalam kutoka Wizara ya Kilimo na Chakula Tanzania.

41. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Programu ndogo hii iliombewa jumla ya **TZS 777.8 milioni** kwa kazi za kawaida (TZS 227.8 milioni Mshahara na TZS **550.00** milioni kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Aprili, 2019 programu imepata **TZS 738.33 milioni** (**TZS 188.33** milioni mishahara na **TZS 550.00** milioni kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 95 ya fedha zilizoombwa.

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA

42. Mheshimiwa Spika, Programu hii inasimamiwa na Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka na ina jukumu la kuwashirikisha wananchi kutunza na kuendeleza raslimali za

misitu na wanyama pori pamoja na kusimamia uhifadhi wa misitu, maliasili zisizorejesheka, mashamba ya Serikali, viumbe hai pamoja na mazingira yao sambamba na kusimamia mahitaji ya soko na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu. Program hii inajumuisha programu ndogo mbili ambazo ni Programu ya Maendeleo na Uhifadhi wa Rasilimali za Misitu na Programu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka.

Programu ndogo ya Maendeleo na Uhifadhi wa Misitu

43. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina lengo la kusimamia na kuhifadhi misitu, wanyama pori pamoja na mazingira yao.

Utekelezaji wa shabaha kwa mwaka 2018/2019

44. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, program imetekeliza yafuatayo:

- a) Miche 1,042,008 imeoteshwa (Unguja 871,043 na Pemba miche 170,965) ikiwemo Mikarafuu 304,660, matunda na viungo 156,516 na misitu 580,832.
- b) Wafugaji 22 wa nyuki wamepatiwa mafunzo ya urinaji na usarifu wa mazao ya nyuki. Washiriki wa mafunzo hayo wametoka katika kamati za uhifadhi za Misitu ya jamii kutoka Shehia za Mtende, Kibuteni, Kitogani na Unguja Ukuu) na wafugaji wazoefu wa nyuki kutoka shehia za Bumbwini, Bungi, Kiwengwa, Bambi, Jambiani, Ng'ambwa, Makunduchi, Chwaka na Uzi.

- c) Mikataba 6 ya usimamizi wa Misitu ya Jamii imetayarishwa na imo katika hatua za mwisho za utiaji wa saini. Mikataba hiyo inajumuisha shehia za Makangale, Kipange, Wingwi mapofu, Wingwi mtemani, Majenzi Micheweni na Kiuyu.
- d) Idara ilishiriki katika Maonesho ya Kimataifa ya Utalii yaliyofanyika katika Hotel ya Verde na ilipata fursa ya kutangaza vivutio vya Utalii kupitia hifadhi nne: Jozani – Chwaka Bay National Park, Masingini, Kiwengwa – Pongwe na Ngezi Vumawimbi Nature Reserve.
- e) Vikao vya majadiliano na Bodi ya Utalii Tanzania Bara (TTB) kwa ajili ya kuweka mikakati ya pamoja katika kuvitangaza vivutio vya utalii vilivyopo katika Hifadhi za Zanzibar vilifanyika.
- f) Doria 169 (Unguja 124 na Pemba 45) zimefanyika na kufanikiwa kukamata na kuteketeza misumeno ya moto 346 (Unguja 206 na Pemba 140). Jumla ya gari 15 za mizigo na gari 15 za ng'ombe zilikamatwa).
- g) Utafiti kuhusu mahitaji na fursa za jamii zinazozunguka Misitu ya Hifadhi Zanzibar kwa Shehia 12 umekamilika. Rasimu ya ripoti ya utafiti imewasilishwa FAO kwa mapitio na maoni yao ili kuikamilisha.
- h) Mapitio ya Mazizi 12 ya wanyamaporu yamefanyika na rasimu ya ripoti ya awali imekamilika; na

i) Kanuni ya Zanzibar juu ya utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Biashara ya wanyamapori, miti na mimea iliohatarini kutoweka (CITES) na kanuni ya mazizi ya wanyamapori zimekamilika na zimo katika hatua ya kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu.

45. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 programu hii iliombewa jumla ya **TZS 2.58 bilioni**. (TZS 2.45 bilioni mishahara na TZS 131.92 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi Aprili, 2019 programu imepata **TZS 1.81 bilioni** (**TZS 1.58 bilioni** mishahara na **TZS 234.77** milioni kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 71 ya fedha zilizoombwa.

Programu ndogo ya Uhifadhi na Usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka

46. Mheshimiwa Spika, Programu hii **inasimamia** na kuratibu matumizi endelevu ya rasilimali zisizorejesheka

Utekelezaji wa shabaha kwa mwaka 2018/2019

47. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, program imetekeleza yafuatayo:

- Hekta 7 (4 Zingwezingwe na 3 Manga Pwani) zimepandwa miti ya misitu msimu wa Vuli 2018/2019;
- Doria 55 (35 Unguja na 20 Pemba) zimefanywa na kukamata matukio 59 ya uchimbaji na usafirishaji maliasili

zisizorejesheka yanayoju muisha (33 Mchanga, 6 Kifusi, 5 Gari za Ng'ombe, 4 Kokoto, 2 Mawe, 5 Matofali ya Jasi na 3 Udongo);

- c) Rasimu za Sera na Sheria za Maliasili zisizorejesheka zimeandaliwa kwa mapitio zaidi.

48. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/19 programu hii iliombewa jumla ya **TZS 357 milioni** kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia Aprili, 2019 programu imepata **TZS 186.95** milioni kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 53 ya fedha zilizoombwa.

PROGRAMU YA MAENDELEO YA MIFUGO

49. Mheshimiwa Spika, Programu ya Maendeleo ya Mifugo jukumu lake kubwa ni kuendeleza sekta ya mifugo na kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo na mazao yake. Programu hii imegawika katika programu ndogo mbili ambazo ni Programu ndogo ya uzalishaji na utabibu wa mifugo Programu ndogo ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo –ZALIRI.

50. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019, Programu ya Maendeleo ya Mifugo ziliombewa jumla ya **TZS 3.66 bilioni** (TZS 1.68 bilioni Mshahara, TZS 300.00 milioni kwa matumizi mengineyo, TZS 828.9 milioni ikiwa ni Ruzuku na TZS 856.00 milioni ni fedha za programu ya miundombinu ya mifugo). Hadi kufikia Aprili, 2019 programu imepata **TZS 2.77 bilioni** (TZS 1.30 bilioni mishahara na TZS 290.6 milioni

kwa matumizi mengineyo na TZS 579.69 milioni ni Ruzuku na TZS 603.20 milioni ni fedha za programu ya miundombinu).

Programu Ndogo ya Uzalishaji wa Mifugo

51. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya uzalishaji wa Mifugo inalenga kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo na mazao yake.

Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2018/2019

52. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, program imetekeliza yafuatayo:

- a) Jumla ya wafugaji 13,221 walitembelewa na kupatiwa ushauri wa kitaalamu wakiwemo 6,770 wa ng'ombe, 1899 wa kuku na 4,552 wa mbuzi;
- b) Ng'ombe 1784 walipandishwa kwa sindano Unguja na Pemba;
- c) Ekari 25 zimeimarishwa kwa kupandwa malisho majani Maruhubi, Kizimbani na Chamanangwe;
- d) Madaktari 40 wa vijijini (CAHWS) wa mifugo wamepatiwa mafunzo msasa.
- e) Vituo vitano (5) vya ukusanyaji na usarifu wa maziwa kwa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa vimeanza kujengwa kupitia programu ya Heifer.

53. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 programu ndogo ya Uzalishaji wa Mifugo iliombewa jumla ya **TZS 1.05 bilioni** (TZS 198.5 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo na TZS 856.00 milioni ikiwa ni fedha za programu ya miundombinu ya mifugo). Hadi kufikia Aprili, 2019 programu imepata **TZS 778.20 milioni** (TZS 175.0 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo na TZS 603.20 milioni ikiwa ni fedha za programu ya miundombinu ya mifugo sawa na asilimia 75 ya fedha zilizoombwa.

Programu Ndogo ya Huduma za Utabibu wa Mifugo

- a) Wanyama 53,543 walichanjwa dhidi ya maradhi tofauti (Ng'ombe 615, mbwa 1,873, Paka 640, Punda 16, na jamii ya kuku 50,399);
- b) Wanyama 33,782 wametibiwa maradhi tofauti (ng'ombe 4,937, mbuzi 1,852, mbwa 8,231, paka 581, Punda 140, sungura 198 na jamii ya kuku 18,527);
- c) Wanyama 17,686 waliogeshwa kwa dawa dhidi ya wadudu wanaosababisha maradhi ya mifugo.

54. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Huduma za Utabibu wa Mifugo iliombewa jumla ya **TZS 1.78 bilioni** kwa kazi za kawaida (TZS 1.68 bilioni Mishahara na TZS 101.5 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo). Hadi kufikia Aprili, 2019 programu imepata **TZS 1.41 bilioni**. (TZS 1.30 bilioni

Mishahara na TZS 115.6 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo) sawa na asilimia 80 ya fedha zilizoombwa.

Programu Ndogo ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo –ZALIRI Utekelezaji wa Shabaha kwa mwaka 2018/2019

55. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Programu hii ilitekeleza shabaha zifuatazo:

- a) Matengenezo makubwa ya ofisi za Taasisi yamekamilika na imeshahamiwa.
- b) Ujenzi wa mabanda mawili ya utafiti wa kuku na mbuzi yamekamilika.
- c) Taasisi imeshiriki mikutano miwili ya mwaka Arusha (Tanzania Society of Animal Production-Octoba 2018 na Tanzania Veterinary Association-Novemba 2018);
- d) Watafiti wawili kutoka Unguja wamepatiwa mafunzo juu ya uandishi wa mapendekezo ya Tafiti zenye ushindani. Vilevile watafiti wasaidizi 5 wa Wilaya ya Mkoani wamepatiwa mafunzo juu ya ukusanyaji wa sampuli za utafiti wa minyoo;
- e) Tafiti mbili zilifanyika na kukamilika kuhusu Tathmini ya uzito na ubora wa nyama ya ng'ombe wanaofugwa Zanzibar na Tathmini ya uzito wa kuku wa nyama wanaotumia chakula cha madukani na kilichotengenezwa na Taasisi). Ripoti za matokeo ya utafiti huu zimekamilika kwa hatua ya

mwanzo na matokeo ya awali yanatarajiwa kutolewa mwezi wa Juni, 2019;

- f) Tafiti nne zinaendelea ambazo ni za tathmini ya mwenendo wa maradhi ya minyoo; ya uzalishaji wa mbuzi wa asili na chotara; matumizi ya mwani katika chakula cha kuku na tathmini ya uzalishaji na kuhifadhi aina tano ya kuku wa asili wa Zanzibar.
- g) Rasimu ya awali ya Sheria ya Kuanzishwa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar imekamilika.

56. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo kwa mwaka wa fedha 2018/2019, iliombewa jumla ya **TZS 828.90 milioni** ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini (TZS 303.90 milioni ni mshahara na TZS 525.00 milioni kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Aprili, 2019 programu imepata **TZS 579.69 milioni** (TZS 202.45 mshahara na TZS 377.24 matumizi ya kawaida) sawa na asilimia 70 ya fedha zilizoombwa.

PROGRAMU YA MAENDELEO YA UVUVI

57. Mheshimiwa Spika, Programu ya Maendeleo ya Uvuvu dhumi lake kubwa ni kuendeleza uvuvi na kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao ya baharini kwa njia ya ufugaji. Programu hii imegawika katika program ndogo mbili ambazo ni: Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvu na Uhifadhi wa Bahari; na Programu ndogo ya Ufugaji wa Mazao ya Baharini.

Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari

58. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa bahari inalenga kuendeleza uvuvi wa kienyeji na kusimamia rasilimali za baharini kwa matumizi endelevu.

Utekelezaji wa Shabaha kwa mwaka 2018/2019

59. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Programu hii ilitekeleza shabaha zifuatazo:

- a) Mafunzo ya sheria ya uvuvi na kanuni za maeneo ya hifadhi yalitolewa kwa wajumbe 67 wa kamati za uvuvi za PECCA na MENAI na wanajamii 40 walipatiwa mafunzo kuhusiana na mambo ya uhifadhi wa ndege waliohatarini kutoweka katika Fungu Mbaraka. Aidha, mikutano ya usuluhishaji wa mgogoro kwa wavuvi wa Mtende na Mzuri, Matemwe na Pwani Mchangani ilifanyika.
- b) Doria shirikishi 174 za baharini na nchi kavu zilifanyika katika maeneo tofauti. Matokeo ya doria yamebainisha kwamba wavuvi 3,839 hawakuwa na leseni na kulazimika kukata leseni;
- c) Wanafunzi 13 (10 MSc na 3 PhD) wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika vyuo vyatia na ndani na nje ya nchi na

wafanyakazi 30 wamepelekwa kwenye mafunzo ya uokozi, takwimu na utawala huko Tanzania Bara;

- d) Mafunzo ya upandaji mwani katika kina kirefu cha maji yalifanyika vijiji 48 (Unguja 16 na Pemba 32).
- e) Mtambo wa kuzalisha barafu umefungwa katika soko la samaki Tumbe na umeanza kazi kwa lengo la kuhifadhi mazao ya baharini mara baada ya kuvuliwa.

60. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019, Programu ndogo hii iliombewa **TZS 20.48 bilioni** (TZS 790.99 milioni ni mishahara, TZS 165.4 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo, TZS 3.92 bilioni kutoka SMZ kwa miradi ya maendeleo na TZS 15.6 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo). Hadi kufikia Aprili, 2019, Programu imepatiwa **TZS 2.27 bilioni** (TZS 681.86 milioni mshahara, TZS 150.00 matumizi mengineyo na TZS 1.44 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) sawa na asilimia 11 ya fedha zilizoombwa.

Programu Ndogo ya Ufugaji wa Mazao ya Baharini

61. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Mazao ya Baharini inalenga kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao mengine ya baharini.

Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2018/2019

62. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Programu hii ilitekeleza shabaha zifuatazo:

- a) Vikundi 144 Unguja na Pemba vilipatiwa taaluma ya mbinu bora za ufugaji na usarifu wa mazao ya baharini.
- b) Vifaranga 9,000 vya majongoo vimezalishwa kati ya hivyo 500 wamepelekwa Uzi kwenye mashamba darasa.
- c) Vikundi 30 vya wakulima na usarifu wa zao la mwani vilipatiwa vifaa vya kulimia mwani (taitai 2,250 na kamba/roli 1,222).

63. Mheshimiwa Spika, kwa waka wa fedha wa 2018/2019, Programu ndogo ya kuimarisha ufugaji wa mazao ya baharini iliombewa **TZS 284.6 milioni** kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Aprili, 2019 programu imepata TZS 225.00 milioni kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 79 ya fedha zilizoombwa.

KAMPUNI YA UVUVI

64. Mheshimiwa Spika, Lengo kuu la Kampuni ya Uvuvi ni kuanzisha Uvuvi wa kibiashara kwa kuimarisha ujenzi wa Miundombinu ya Uvuvi na kuelekeza nchi yetu katika uchumi wa Buluu.

Utekelezaji wa Shabaha Kampuni ya Uvuvi ya ZAFICO 2018/2019

Kampuni imeweza kutekeleza shabaha zifuatazo:

- a) Kampuni imeweza kuandaa Mpango wake wa Biashara wa miaka mitano (Five years Business Plan) na kupendekeza juu

ya aina gani za biashara ZAFICO inaweza kuanza nazo kwa kipindi hicho;

- b) Kampuni pia imeweza kukamilisha Utafiti wa Masoko ya ndani na nje ya Zanzibar kwalengo la kujipanga vyema kibiashara kutokana na bidhaa itakazozizalisha au huduma itakazozitoa;
- c) Kufikiwa kwa hatua za mwisho za manunuzi ya Boti ya Uvuvia ina ya “Longliner” kutoka nchini Srilanka na kutarajiwu kuanza shughuli zake za Uzalishaji katikati mwa Mwezi Juni 2019.
- d) Kukamilika kwa zoezi la Upembuzi yakinifu, Tathmini ya ujenzi na Michoro ya eneo linalotarajiwa kujengwa upya mitambo ya baridi kwa ajili ya kuhifadhi samaki na uzalishaji wa barafu lililokuwepo bandari ya Malindi, Zanzibar.
- e) Kukamilika kwa Utafiti bainishi (Feasibility study) kwa ajili ya uanzishwaji wa shamba la kufugia samaki baharini eneo la Mkokotoni Kaskazini Unguja.
- f) Jumla ya wafanyakazi wanne (4) wa Kampuni wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi (Wahasibu 2, Mshika fedha 1 wamepatiwa mafunzo “Business accounting” na Quick book accounting”) na (Mwanasheria wa Kampuni/Katibu wa Bodi kupatiwa mafunzo ya Ukatibu wa bodi za Kampuni)

g) Jumla ya wavuvi 40 na wakuu wa Madiko 4 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi juu ya matumizi ya Kifaa maalumu cha kuweza kufatilia nyenendo zao za mavuvi wakiwemo bahari (Automatic Identification System – AIS) kwa lengo la kujua ni maeneo gani hasa shughuli za uvuvi wa dagaa unafanyika kwa kiwango kikubwa. Lakini pia kifaa hicho hutumika kwa shughuli za uokozi pindi mvuvi atakapotokezewa na dharura.

65. Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) ilitegemewa kutumia Jumla ya TZS 7.0 bilioni zitakazochangiwa na mashirika ya ndani ya Zanzibar ikiwemo ZSSF -TZS 3.1 bilioni sawa na asilimia 45 ya hisa, ZSTC –TZS 1.9 bilioni sawa na asilimia 27 ya hisa, BIMA - TZS 700.00 milioni sawa na asilimia 10 ya hisa na Shirika la Bandari - TZS 1.26 bilioni sawa na asilimia 18 ya hisa. Hadi kufikia Aprili, 2019 Kampuni imetumia TZS 1,311,867,646 bilioni kwa kazi za kampuni sawa na asilimia 19 ya fedha zilizoombwa.

PROGRAMU YA UTAWALA, MIPANGO NA USIMAMIZI WA KAZI ZA WIZARA

66. Mheshimiwa Spika, Programu hii inayojumuisha programu ndogo tatu ambazo ni Programu Ndogo ya Mipango na Usimamizi wa Kazi za Wizara na Programu ndogo ya Utawala.

Programu Ndogo ya Mipango na Usimamizi wa Kazi za Wizara

67. Mheshimiwa Spika, dhumiuni la Programu hii ni kusimamia na kuratibu Sera, Sheria, Mikakati, Mipango ya Maendeleo na Utafiti, pamoja na kuratibu mashirikiano ya Wizara na taasisi za ndani na nje ya nchi **ikiwemo** Washirika wa Maendeleo na Sekta Binafsi. Programu hii inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2018/2019

68. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Programu hii ilitekeleza shabaha zifuatazo:

- a) Ukusanyaji wa takwimu za mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na maliasili umefanyika kwa kushirikiana na Maofisa wa Wilaya;
- b) Usimamizi na tathmini ya utekelezaji wa Miradi na Programu za Wizara imefanyika;
- c) Utayarishaji wa nyaraka na tarifa mbali mbali za utekelezaji wa majukumu ya Wizara umefanyika na kuziwasilisha kwa wadau;

- d) Ufutiliaji na tathmini wa kazi za Wizara ikijumuisha uandishi wa ripoti zilifanyika. Aidha, maofisa wawili wapya wa kitengo cha Ufutiliaji na Tathmini walipatiwa mafunzo maalumu ya siku mbili. Mafunzo hayo yalitolewa na mtaalamu kutoka Tume ya Mipango;
- e) Ukusanyaji na mapitio ya tafiti za Wizara umefanyika;
- f) Maofisa wa Idara ya Mipango walishiriki katika mikutano sita (6) ya mashirikiano na Wizara za Sekta ya Kilimo Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;
- g) Nakala 500 za jarida la Kilimo zimetayishwa na kuchapishwa;
- h) Rasimu ya Programu Maendeleo ya Sekta ya Kilimo iliwasilishwa kwa Kamati ya Uongozi ya Wizara, Makatibu Wakuu na Baraza la Mapinduzi.
- i) Sera na Sheria ya Minazi zimetayarishwa, Sera ya Kilimo ya mwaka 2002 inafanyiwa mapitio kwa kushirikiana na Shirika la Chakula – FAO.

69. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019, programu ndogo ya Mipango iliombewa jumla ya **TZS 10.75 bilioni** (TZS 343.7 milioni mishahara, TZS 400.00 milioni kwa matumizi mengineyo, TZS 380.0 milioni kutoka SMZ kwa ajili ya Miradi ya maendeleo na TZS 9.63 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo). Hadi kufikia Aprili, 2019 programu

imepata jumla ya **TZS 3.39 bilioni** (TZS 251.34 milioni mishahara; TZS 395.00 milioni matumizi mengineyo; (**TZS 2.36 bilioni** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS 380.00 milioni kutoka SMZ) sawa na asilimia 31.5 ya fedha zilizombwa.

Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji

70. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya utawala na uendeshaji imetekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Madhumuni ya programu hii ni kusimamia rasilimali watu na kutoa huduma za utawala katika Wizara, ikiwa ni pamoja na masuala ya ajira, mafunzo, maslahi ya wafanyakazi na uwekaji wa kumbukumbu. Aidha, programu inaratibu masuala mtambuka ikiwemo Ukimwi, jinsia, kusimamia utunzaji na uhifadhi wa mali za Serikali, utoaji wa huduma za manunuzi na uhifadhi wa vifaa.

Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2018/2019

71. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Programu hii ilitekeleza shabaha zifuatazo:

- a) Jumla ya magari 63 na pikipiki 217 zimehakikiwa na kupatiwa usajili;
- b) Wafanyakazi 504 wamepatiwa maaslahi yao, (398 wamepatiwa fedha za likizo, 82 fedha za muda wa ziada, 22 fedha za ubani na watatu (3) fedha ya matibabu ndani ya nchi. Jumla ya wafanyakazi 119 wamejengewa uwezo wa

kitaaluma kati ya hao, wafanyakazi 24 wamepatiwa mafunzo ya ndani na nje ya nchi ambapo wafanyakazi wanane (8) wapo katika kiwango cha Shahada ya pili (Master), mmoja (1) Stashahada ya Uzamili (Post Graduate), kumi na moja (11) Shahada ya kwanza (Degree), wanne (4) Stashahada (Diploma). Aidha Wastaafu watarajiwa 70 wamepatiwa mafunzo kuhusiana na kujiandaa kustaaafu na ujasiriamali, Pia wafanyakazi (5) wamepatiwa mafunzo ya muda mafupi pamoja na wafanyakazi (20) wamepatiwa mafunzo ya kuthibitishwa kazi;

- c) Kitengo cha Wakaguzi wa Ndani kimehakiki mapato na matumizi ya Serikali kwa kila kipindi cha miezi mitatu katika Idara na taasisi zilizo chini ya Wizara;
- d) Kitengo cha Manunuvi cha Wizara kimefanya vikao 32 vya zabuni na tathmini ya manunuvi ya vifaa na huduma kwa kampuni kupitia miradi na taasisi za zake;
- e) Wizara imekamilisha suala la ugatuvi wa wafanyakazi 618 na kuwahamishia katika Wizara ya Nchi Ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kutoka katika Idara ya Misitu, Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Umwagiliaji;
- f) Kitengo cha habari na mawasiliano cha Wizara kimeandaa matangazo ya redio, TV, makala na vijarida kwa kushirikiana na vyombo vya habari ikiwemo ZBC, ITV, TIF TV, TBC, Bahari FM na vyombo vyengine.

72. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya utawala na mafunzo, kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019, iliombewa jumla ya **TZS 2.52 bilioni** kwa kazi za kawaida (TZS 1.83 bilioni ni mishahara na TZS 688.00 milioni kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Aprili, 2019 programu imepatiwa **TZS 2.03 bilioni** (TZS 1.35 bilioni kwa mishahara na TZS 685.00 milioni kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 81 ya fedha zilizoombwa.

Programu Ndogo ya Uratibu wa Kazi za Wizara Pemba

73. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya uratibu Ofisi Kuu Pemba, kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019 iliombewa jumla ya **TZS 3.37 bilioni** (TZS 3.30 bilioni mishahara na TZS 70.00 milioni ni matumizi mengineyo). Hadi kufikia Aprili, 2019 programu imepata **TZS 2.79 bilioni** (TZS 2.74 bilioni mishahara na TZS 57.9 milioni matumizi mengineyo) sawa na asilimia 83 ya fedha zilizoombwa.

CHANGAMOTO

74. Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Wizara na Serikali kwa ujumla, baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza malengo yaliyowekwa ni pamoja na:

- a) Uvamizi wa ardhi za kilimo na misitu kutokana kuongezeka kwa makaazi na miradi mengine ya maendeleo
- b) Kuongezeka kwa bei ya pembejeo za Kilimo

- c) Wakulima kuchelewa na kutokuchangia katika kupatiwa huduma za matrekta
- d) Kuendelea kuwepo kwa matumizi mabaya ya msumeno wa moto.
- e) Kuwepo kwa nzi wa matunda.
- f) Kuongezeka kwa mahitaji ya matumizi ya mchanga pamoja na kupungua kwa maeneo ya uchimbaji.

HATUA ZINAZOCHUKULIWA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

- a) Wizara inaendelea kushirikiana na Wizara ya Ardhi kuyatambua, kuyapima na kuyapatia Hati Miliki maeneo ya Kilimo.
- b) Wizara inaendelea kufuatilia utaratibu mzuri wa ununuzi wa pembejeo kwa njia ya ujumla (bulk purchase) kutoka viwandani au kupitia kwa Wakala wa Mbolea Tanzania na China;
- c) Wizara inaendelea kushajiisha wakulima kuendelea kuchangia huduma za matrekta kwa wakati.
- d) Wizara inaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na udhibiti na matumizi ya msumeno wa moto. Aidha, Wizara inaendelea kuimarisha doria sambamba na kuangamiza misumeno inayokamatwa.

- e) Wizara inaendelea na jitihada ya kutoa elimu kwa wakulima sambamba na kuwashajiisha kutumia mbinu mbadala za kuwaangamiza wadudu waharibifu wa matunda.
- f) Kuimarisha udhibiti wa matumizi ya rasilimali zisizorejesheka kwa kuandaa utaratibu maalumu wa upatikanaji wa rasilimali hizo. Aidha, Wizara inaendelea na tafiti ya kuainisha mahitajihalisi nakiwango cha rasilimali hizo zilizopo;
- g) Kuendeleza utafiti mashambani (On farm research).

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

MAKADIRIO YA MAPATO 2019/2020

75. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020, Wizara imekadiria kukusanya mapato ya jumla ya **TZS 10.46 bilioni** kutoka vianzio vyake 12 vya Unguja na Pemba (**Kiambatisho nam. 5**).

MAKADIRIO YA MATUMIZI 2019/2020

76. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 itatekeleza malengo yake kupitia programu zake kuu tano ambazo ni:

- a) Programu ya Maendeleo ya Kilimo;

- b) Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu na Maliasili Zisizorejesheka;
- c) Programu ya Maendeleo ya Mifugo;
- d) Programu ya Maendeleo ya Uvuvi; na
- e) Programu ya Mipango na Utawala wa Kazi za Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Aidha, Wizara itaendelea na utekelezaji wa miradi na Programu 12 za maendeleo ikiwemo SWIOFish, ERPP, Agri-Connect, TANIPAC, Climate Smart Agriculture, Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Maji, Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Sekta ya Kilimo, Mradi wa Kuendeleza Utafiti wa Mifugo, Mradi wa Kutotolea Vifaranga vya Samaki na Mradi wa Usimamizi wa Matumizi wa Misitu ya Mwambao na MIVARF, Ujenzi wa Soko la Malindi.

77. Mheshimiwa Spika, kwa kutekeleza programu hizo kwa mwaka wa fedha wa 2019/20 Wizara imekadiriwa kutumia jumla ya **TZS 88.17 bilioni** kati ya fedha hizo **TZS 22.98 bilioni** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS 11.42 bilioni Mishahara na TZS 5.70 bilioni matumizi mengineyo na TZS 5.86 bilioni RUZUKU kutoka SMZ kwa ajili ya Chuo cha Kilimo Kizimbani, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo (**Kiambatisho nam. 6**). Kwa kutekeleza programu na Miradi ya

Maendeleo Wizara imetengewa **TZS 65.19 bilioni** (**TZS 60.26 bilioni** kutoka kwa washirika wa maendeleo na **TZS 4.93 bilioni** kutoka SMZ (**Kiambatisho nam.7**).

78. Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zinazochukuliwa na Wizara katika kuendeleza kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 imejiwekea malengo yafuatayo kupitia programu zake tano:

- a) Kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji hekta 500 (mabwawa 2, visima 16 pamoja na mitaro ya umwagiliaji) kupitia mradi wa EXIM BANK wa Korea, 65 kupitia mradi wa ERPP pamoja na kukarabati hekta 87.
- b) Kufuatilia uzalishaji wa mpunga katika eneo la ekari 33,800 (20,800 Pemba na Unguja 13,000) pamoja na mazao mengine ya kilimo;
- c) Kushajiisha matumizi ya pembejeo kwa kununua na kusambaza tani 800 za mbolea, lita 21,000 za dawa ya kuulia magugu na tani 200 za mbegu ya mpunga;
- d) Kuendelea na tafiti 12 (8 Kilimo na 4 Mifugo), kuanzisha tafiti 12 mpya (5 Uvuvi, 5 Kilimo na 2 Mifugo), kuchapisha ripoti za tafiti zilizokamilika na kutoa mafunzo kwa watafiti.
- e) Kuendeleza uoteshaji wa miche 1,800,000 kwa kutumia teknolojia ya kisasa ikiwemo Mikarafuu; Misitu, matunda na

mapambo, pamoja na upandaji miti 250,000 katika mashamba ya Serikali Unguja na Pemba;

- f) Kufanya tathmini na kuhakiki aina za mimea zinazozalishwa Zanzibar;
- g) Kushajiisha wazalishaji wa asali na kuwapatia taaluma bora ili waongeze uzalishaji kutoka tani 9 hadi 15.
- h) Kuimarisha huduma za kinga na tiba dhidi ya wanyama;
- i) Kuimarisha miundombinu ya utafiti na uzalishaji wa mifugo;
- j) Kuimarisha huduma za upandishaji ng'ombe 5,000 kwa sindano Unguja Pemba.
- k) Kuzalisha vifaranga vyta samaki 1,000,000 kaa 75,000, na majongoo 50,000 na kuvisambaza kwa vikundi vyta wafugaji Unguja 51 na Pemba 93;
- l) Kuandaa Mpango Mkakati wa Uendelezaji wa Sekta ya Mifugo;
- m) Kuimarisha uvuvi unaozingatia uhifadhi wa mazingira ya baharini kwa kamati 88 za uvuvi (Unguja 55 na Pemba 33);
- n) Kuongeza mashamba ya mfano manne (4) ya uzalishaji wa kaa, samaki na majongoo ya pwani Unguja na Pemba;
- o) Kufanya utafiti wa bei za vyakula na kutoa bei elekezi kwa kilo kwa baadhi ya mazao ya chakula pamoja na uchunguzi

wa kutambua hatari za usalama wa chakula katika minyororo ya thamani ya mboga na matunda;

- p) Kutoa maslahi kwa wafanyakazi 1,200 ikiwemo malipo ya likizo, muda wa ziada na pesa za ubani kwa wafiwa pamoja na kuwawekea mazingira mazuri ya kazi;
- q) Kupima mashamba matatu (kilombero, Pangeni na Wesha Pemba) na kuyapatia hatimiliki;
- r) Kutayarisha mpango mkakati wa ukusanyaji, uchambuzi na utoaji wa takwimu za sekta ya kilimo;
- s) Kutekeleza programu ya kuendeleza zao la nazi Zanzibar;
- t) Kufanya tafiti tatu za kiuchumi na kijamii Unguja na Pemba na kufanya mikutano miwili (2) ya Baraza la Utafiti la sekta ya kilimo;
- u) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo Zanzibar Z-ASDP.

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO

79. Mheshimiwa Spika, Programu ya Maendeleo ya Kilimo Programu hii imegawika katika programu ndogo nne ambazo ni:

- a) Programu ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji Maji;
- b) Programu ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo;

- c) Programu ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Serikali wa Huduma za Matrekta.
- d) Programu ndogo ya Uhakika wa Chakula na Lishe.

80. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020, Programu ya Maendeleo ya Kilimo inaombewa jumla ya **TZS 44.5 bilioni** kati ya fedha hizo **TZS 3.5 bilioni** matumizi mengineyo, **TZS 2.38 bilioni** ni Mishahara na **TZS 4.75 bilioni** ni Ruzuku kwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, Chuo cha Kilimo Kizimbani na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na zana za Kilimo. Vilevile, Programu inaombewa jumla ya **TZS 33.86 bilioni** kwa miradi ya maendeleo (TZS 32.86 bilioni kutoka kwa Washirika wa maendeleo na TZS 1.00 bilioni kutoka SMZ).

Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji Maji kwa Mwaka 2019/2020

81. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Programu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

- a) Usimamizi na ufuatiliaji wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji utakaoendeleza hekta 500 katika mabonde ya Kinyasini, Chaani na Kibokwa kuititia mradi wa EXIM BANK wa Korea.

- b) Ulipaji wa fidia ya mazao kwa wakulima watakaoathirika wakati wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika mabonde ya Makwararani, Mlemele na Kinyasini.
- c) Upimaji wa mabonde yatakayoendelezwa miundombinu ya umwagiliaji maji kwa kupata idadi ya wakulima na ukubwa wa maeneo yao wanayolima.
- d) Kuwajengea uwezo kwa kutoa mafunzo kwa wataalamu na jumuiya za wakulima katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji na kusimamia ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji.

82. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Programu ndogo hii inaombewa jumla ya **TZS 34.72 bilioni** ambapo (TZS 560.07 milioni Mshahara, TZS 300.00 milioni kwa matumizi mengineyo, TZS 1.00 bilioni fedha za maendeleo kutoka SMZ na TZS 32.86 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo EXIM BANK.

Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo kwa Mwaka 2019/2020

83. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Programu Ndogo hii ina sehemu mbili ambazo ni Utafiti na ile ya Mafunzo ya Kilimo. Programu Ndogo hii inalenga kutekeleza yafuatayo:

- a) Kufanya tafiti sita (6) mpya za (mpunga 2, muhogo 1, mboga mboga 2, na Uchuguzi wa udongo 1) na kuendeleza tafiti nane (8) za zamani;
- b) Kukarabati jengo moja la Maabara Matangatuani Pemba na kuanza kuweka uzio wa miti hai kuzunguka eneo la Kizimbani, kukarabati nyumba za wafanyakazi Kizimbani na Matangatuani na Kununua vifaa na madawa kwa ajili ya maabara;
- c) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watafiti 10;
- d) Kushiriki katika Maonesho ya Kilimo ya Nane Nane, Siku ya Chakula Duniani na Maonesho ya Biashara Zanzibar;
- e) Kuandika upya Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa kilimo na Kupitia Mpango Mkakati wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo;
- f) Kuimarishe maeneo ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Kizimbani kwa kuyapima na kupanga matumizi yake;
- g) Kuendeleza mashirikiano na Taasisi za utafiti za Ndani, Kikanda na Kimataifa.

84. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Taasisi ya Utafiti inaombewa jumla ya **TZS 2.46 bilioni** (TZS 1.86 bilioni Mshahara na 600.00 milioni kwa matumizi mengineyo).

Shabaha Zitakazotolewa na Chuo cha Kilimo Kizimbani kwa Mwaka 2019/2020

- a) Kuendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi wapya 230 (100 ngazi ya Stashahada na 130 ngazi ya Astashahada);
- b) Kufanya tathmini ya uzalishaji wa mpunga katika skimu ya Uzini na Kianga kwa kushirikiana na Mradi wa TANRICE II;
- c) Kutoa mafunzo ya kilimo bora cha mpunga wa Umwagiliaji maji na wa kutegemea mvua kwa wakulima 100. Mafunzo haya yatatolewa kwa kushirikiana na mradi wa TANRICE II.

85. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Programu inaombewa **TZS 880.0 milioni** ikiwa ni Ruzuku (TZS 757.70 milioni Mishahara na TZS 122.30 milioni matumizi mengineyo).

Shabaha Zitakazotolewa na Programu ndogo ya Kilimo Mwaka 2019/2020

- a) Kununua na kusambaza tani 200 za mbegu ya mpunga, tani 800 za mbolea (TSP tani 300 na UREA tani 500), lita 21,000 za dawa ya kuulia magugu na lita 400 za dawa ya kunasia nzi waharibifu wa matunda;
- b) Kutoa elimu ya uzalishaji katika zao la mpunga kuitia mabonde 10 ya mpango (6 Unguja na 4 Pemba);

- c) Kufuatilia uzalishaji wa mpunga eneo la ekari 33,800 (20,800 Pemba na Unguja 13,000);
- d) Kusambaza mbegu ya muhogo na viazi lishe kwa wakulima 500;
- e) Kutoa huduma za utibabu wa mimea, karantini na ukaguzi wa mazao yanayoingia na kutoka nje ya nchi ikiwemo karafuu;
- f) Kuendeleza uzalishaji wa mazao ya viungo kwa ajili ya usafirishaji nje ya nchi ikiwemo Vanilla, Pilipili Hoho, Manjano, Tangawizi na Pilipili Manga katika hekta tano za mashamba ya mipira Unguja na Pemba.

86. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Programu inaombewa. **TZS 4.30 bilioni** kwa kazi za kawaida (TZS 1.60 bilioni ni Mishahara na TZS 2.70 bilioni matumizi mengineyo).

Shabaha Zitakazotolewa na Wakala wa Serikali na Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo kwa Mwaka 2019/2020

- a) Kusimamia na kurahisisha upatikanaji na matumizi ya zana za kisasa za kilimo zitakazopelekea kuongeza ufanisi katika uzalishaji wa mazao ya kilimo;
- b) Kutoa huduma za matrekta na zana zake kwa wakulima, sekta binafsi na taasisi nyengine;

- c) Kutengeneza matrekta na zana zake na kuhakikisha kuwepo kwa vifaa vya kazi na vipuri kwa ajili ya huduma;
- d) Kutoa mafunzo kwa madereva 35 (20 Unguja na 15 Pemba) na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wasimamizi wa huduma za matrekta mashambani.

87. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Programu ndogo hii inaombewa jumla ya **TZS 1.42 bilioni** ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini (TZS 614.8 milioni ni mshahara na TZS 800.90 milioni kwa matumizi mengineyo).

Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Uhakika wa Chakula na Lishe kwa Mwaka 2019/2020

88. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, programu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

- a) Kuendeleza mafunzo ya lishe kwa wanajamii katika Shehia 100 za Wilaya ya Mciheweni, Chake chake na Kaskazini “A”;
- b) Kufanya ukarabati wa ghala moja liliopo Pemba kwa ajili ya hifadhi ya chakula;
- c) Kufuatilia hali ya chakula nchini;
- d) Kuandaa mikutano ya wadau kuhusiana na masuala ya uhakika wa chakula na lishe.

e) Kuratibu uendeshaji wa ghala la akiba ya chakula Unguja
pamoja na kuweka vifaa na mchele tani 333;

89. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020
Programu ndogo hii inaombewa jumla ya **TZS 721.35 milioni**
kwa kazi za kawaida (TZS 221.35 milioni Mshahara na TZS
500.00 milioni kwa matumizi mengineyo).

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASLIMALI ZA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA

90. Mheshimiwa Spika, Programu ya Maendeleo ya Rasilimali
za misitu na maliasili zisizorejesheka imegawika katika
programu ndogo mbili ambazo ni:

- a) Uhifadhi na Maendeleo ya Misitu;
- b) Usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka.

91. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020,
Programu ya Maendeleo ya Misitu inaombewa jumla ya **TZS
2.29 bilioni** kwa kazi za kawaida (TZS 1.67 bilioni ni mishahara
na TZS 391.80 milioni matumizi mengineyo). Aidha, TZS 228.2
milioni kwa miradi ya maendeleo kutoka SMZ.

**Shabaha zitakazotolewa na programu ndogo ya uhifadhi na
maendeleo ya misitu kwa mwaka 2019/2020.**

92. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020,
programu hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

- a) Kuotesha miche 2,500,000 (1,000,000 Mikarafuu; 1,000,000 Misitu; 200,000 Minazi na 300,000 ya matunda na viungo) katika vitalu vya Serikali;
- b) Kuhamasisha wafugaji 200 wa nyuki juu ya usarifu wa bidhaa za asali, kukabiliana na wadudu wavamizi katika mizinga pamoja na kuwaorodhesha kwa lengo la kujua idadi yao na tani za asali zinazozalishwa;
- c) Kufanya mapitio ya mikataba 18 ya usimammizi wa misitu ya jamii (CoFMA);
- d) Kuhamasisha uekezaji na kutangaza vivutio vya utalii wa kimaumbile ndani na nje ya Zanzibar ili kufikia Watalii 45,000;
- e) Kufanya doria 500 katika maeneo ya maliasili kwa lengo kudhibiti matukio ya uhalifu.
- f) Kufanya utafiti na tathmini ya matumizi ya rasilimali za misitu ya jamii.
- g) Kupandisha hadhi maeneo mawili ya misitu ya jamii (Mtambwe Pemba na Uzi-Vundwe Unguja) na kuwa misitu ya hifadhi;
- h) Kuyatambua na kusajili mazizi ya wanyama pori pamoja kukamilisha kanuni za kusimamia mazizi ya wanyama hao.

- i) Kutayarisha muongozo wa uhifadhi wa Makobe katika kisiwa cha Changuu.

93. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Programu hii inaombewa jumla ya **TZS 114.6 milioni** kwa kazi za kawaida na 228.2 Fedha za Washirika wa Maendeleo.

Shabaha zitakazotolewa na programu ndogo ya uhifadhi na usimamizi wa maliasili zisizorejesheka 2019/2020

94. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina lengo la kuhifadhi na kusimamia maliasili zisizorejesheka kwa kuratibu maeneo yote ya uchimbaji mawe, kokoto, mchanga, udongo pamoja na matofali ya mawe.

Shabaha Zitakazotolewa na Program Ndogo ya Usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka kwa Mwaka 2019/2020

- a) Kurejeshea kwa kupanda miti hekta 40 katika maeneo ya uchimbaji Maliasili Zisizorejesheka;
- b) Kukamilisha Sera na Sheria ya Maliasili Zisizorejesheka;
- c) Kufanya utafiti juu ya namna bora ya urasimishaji na usimamizi katika uchimbaji wa kifusi, mawe na usagaji wa kokoto;
- d) Kufanya utafiti wa kuangalia namna bora ya upatikanaji wa mchanga nchini;

e) Kutathmini mazao na vipando vilivyopo katika maeneo yatakayopendekezwa kuchimbwa mchanga.

95. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Programu ndogo hii inaombewa jumla ya **TZS 1.95 bilioni** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. (TZS 1.67 bilioni ni mishahara na TZS 277.27 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo).

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MIFUGO

96. Mheshimiwa Spika, Programu ya Maendeleo ya Mifugo ina jukumu la kuendeleza sekta ya mifugo na kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo na mazao yake.

Programu imegawika katika Programu Ndogo Mbili

a) Programu ndogo ya uzalishaji mifugo

b) Programu ndogo ya huduma za utabibu wa mifugo

97. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020, Programu ya Maendeleo ya Mifugo inaombewa jumla ya **TZS 3.81 bilioni** (TZS 1.30 bilioni Mshahara, TZS 254.81 milioni kwa matumizi mengineyo, TZS 862.8 milioni ikiwa ni Ruzuku. TZS 194.60 milioni fedha za Mradi wa Miundombinu ya Mifugo na TZS 1.2 bilioni ni fedha za programu ya Utafiti wa Mifugo kutoka SMZ).

Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Uzalishaji wa Mifugo kwa Mwaka 2019/2020

- a) Kuandaa Mpango mkakati wa maendeleo ya mifugo.
- b) Kupandisha ng'ombe 4,000 kwa sindano (Unguja 2,000 na Pemba 2,000);
- c) Kujenga mitambo 4 ya biogas Unguja na Pemba;
- d) Kuimarisha malisho kwa kupanda majani katika eneo la Kizimbani;
- e) Kuendeleza huduma za upandishaji ng'ombe kwa sindano;
- f) Kuwaendeleza madaktari wa mifugo vijiji (CAHWS);
- g) Kutoa elimu na kuziendeleza skuli za wakulima za mazao na mifugo.

98. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Uzalishaji wa Mifugo inaombewa jumla ya **TZS 303.56 milioni** (TZS 108.97 kwa ajili ya matumizi mengineyo na TZS 194.60 milioni fedha za Mradi wa Miundombinu ya Mifugo kutoka SMZ).

Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Huduma za Utabibu wa Mifugo kwa Mwaka 2019/2020

- a) Kuchanja kuku 600,000 dhidi ya ugonjwa wa mahepe Unguja na Pemba;

- b) Kuchanja mbwa 11,000 dhidi ya kichaa cha mbwa (8,000 Unguja na 3,000 Pemba);
- c) Kutoa huduma ya maabara ya mifugo;
- d) Kuimarisha huduma za kinga na tiba.

99. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Huduma za Utabibu wa Mifugo inaombewa jumla ya **TZS 1.45 bilioni** kwa kazi za kawaida (TZS 1.30 bilioni Mishahara na TZS 145.85 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo).

Programu Ndogo ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo

100. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Programu ndogo ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (ZALIRI) inalenga kutekeleza shabaha zifuatao:

- a) Kufanya tafiti sita (6) za Mifugo Unguja na Pemba;
- b) Kuimarisha miundombinu ya Taasisi ya Utafiti;
- c) Kuchapisha na kuhifadhi taarifa za matokeo manne ya utafiti uliokamilika;
- d) Kuimarisha mahusiano ya Taasisi za ndani, Kikanda, Kitaifa na Kimataifa na wadau wa sekta ya Mifugo; na
- e) Utayarishaji wa Sheria ya Uanzishwaji Taasisi ya Utafiti wa Mifugo.

101. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, inaombewa jumla ya **TZS 2.06 bilioni** ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini (TZS 305.70 milioni ni mshahara na TZS 556.50 milioni kwa matumizi mengineyo na TZS 1.20 bilioni fedha za Maendeleo kutoka SMZ).

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI

102. Mheshimiwa Spika, Programu ya Maendeleo ya Uvuvu dhumuni lake kubwa ni kuendeleza uvuvi na kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao ya baharini kwa njia ya ufugaji. Programu hii inaombewa jumla ya **TZS 19.83 bilioni** (TZS 763.80 milioni ni Mishahara, TZS 378.20 milioni ni matumizi mengineyo na TZS 250.00 milioni ni Ruzuku kwa Taasisi ya Utafiti ya Uvuvu ambayo imeanzishwa hivi karibuni. Aidha, TZS 1.65 bilioni kwa miradi ya maendeleo kutoka SMZ na TZS 16.78 bilioni kutoka kwa Washirika wa maendeleo).

Programu imegawika katika Programu Ndogo Mbili

- a) Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvu na hifadhi za Baharini
- b) Programu Ndogo ya Kuimarisha Ufugaji wa Mazao ya Baharini

Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvu na hifadhi za Baharini

103. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na hifadhi za baharini inalenga kuendeleza uvuvi wa kienyeji na kusimamia rasilimali za baharini kwa matumizi endelevu. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Programu ndogo hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

- a) Kuendelea kuwajengea uwezo wa kitaaluma Wafanyakazi 8 ili kuimarisha taaluma za uvuvi;
- b) Kuimarisha doria shirikishi 174 katika maeneo ya hifadhi Unguja na Pemba;
- c) Kujenga ofisi mbili za maeneo ya hifadhi za baharini (CHABAMKA na TUMCA);
- d) Kujenga Chelezo katika eneo la Kampuni ya Uvuvi - ZAFICO;
- e) Kujenga maabara ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na mazao ya Baharini;
- f) Kuimarisha uvuvi unaozingatia uhifadhi wa mazingira wa kamati 91za uvuvi Unguja na Pemba;
- g) Kusimamia ujenzi wa soko kuu la samaki linalojengwa diko la Malindi;
- h) Kutoa huduma zitakazolenga kuingia katika uvuvi wa viwanda kwa ajili ya kupata tija zaidi na kuinua kipato cha wavuvi.

104. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020, Programu ndogo hii inaombewa **TZS 19.4 bilioni** (TZS 763.78 milioni ni mishahara, TZS 200.00 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo, TZS 1.65 bilioni kutoka SMZ kwa miradi ya maendeleo na TZS 16.78 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo). Aidha, kwa mwaka 2019/20 program itasimamia miradi ya SWIOfish na Mradi wa Kuimarisha Ufugaji wa Mazao ya Baharini (**Kiambatisho 8a & 8b**)

Programu Ndogo ya Kuimarisha Ufugaji wa Mazao ya Baharini

105. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya mazao ya baharini inalenga kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao mengine ya baharini.

Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo hii:

- a) Kutoa taaluma ya mbinu bora za ufugaji, usarifu, ujasiriamali wa mazao ya baharini na kilimo cha mwani kwa vikundi 144 Unguja na Pemba;
- b) Kuzalisha vifaranga vya samaki milioni 10, kaa 70,000 na majongoo 50,000 na kuwasambaza kwa wananchi;
- c) Kusambaza vifaa kwa vikundi 30 vya wakulima wa zao la mwani;
- d) Kusimamia ukaguzi na usafirishaji wa mazao ya baharini;
- e) Kuendeleza ukulima wa mwani katika maji ya kina kirefu.

106. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020, Programu hii ndogo ya kuimarisha ufugaji wa mazao ya baharini inaombewa **TZS 178.2 milioni** kwa matumizi mengineyo.

Kampuni ya Uvuvi –ZAFICO

107. Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Uvuvi ZAFICO kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Programu ndogo hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

- a) Kukamilisha taratibu zote za ununuzi wa Boti ya Uvuvi, vibali vya ruhusa kwa ajili ya shughuli za uvuvi, Bima pamoja na Mafunzo kwa wavuvi wa boti hiyo mpya ya ZAFICO Kutokea Srilanka;
- b) Kuanza mchakato wa manunuzi wa Boti nyengine mpya ya Uvuvi kutokea nchini Maldives;
- c) Kuanza shughuli za Ujenzi wa eneo la Mitambo ya baridi kwa ajili ya kuhifadhi samaki na kuzalisha barafu;
- d) Kufanya Utafiti bainishi (Feasibility study) katika mnyororo mzima wa biashara ya madagaa Zanzibar;
- e) Kuanza biashara ya ukaushaji na usafirishaji wa Dagaal;
- f) Kukamilisha taratibu na kuanza ujenzi wa eneo la mitambo ya baridi kwa ajili ya uhifadhi wa samaki na uzalishaji wa barafu;

- g) Kukamilisha taratibu za kisheria na kitafiti ili kuanzisha Shamba la ufugaji wa samaki baharini katika eneo la Mkokotoni Kaskazini Unguja;
- h) Jumla ya wafanyakazi 25 wa Kampuni (15 wakijumuisha, Msimamizi wa Misafara ya Boti 1, Manahodha2, Wahandisi 2 na Mabaharia 10 kwa awamu ya kwanza na Maafisa 5 na Wahudumu wa Kampuni 5 kwa awamu ya pili) watapatiwa mafunzo ya muda mfupi ili kuimarisha uwezo wao wa kazi kwa mujibu wa Kada zao katika Kampuni.

108. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Kampuni ya Uvuvi ZAFICO inatarajia kuingiziwa jumla ya **TZS 9.8 bilioni** ikiwa ni pato litokanalo na mchango wa wana Hisa wake (ZSSF, ZSTC, ZIC na ZPC) pamoja na pato litakalotokana na uzalishaji wake kwa kipindi hicho. Aidha, inatarajiwa kutumia jumla ya TZS. 9.6 bilioni (TZS. 3.2 bilioni Shughuli za kawaidana TZS. 6,4 bilioni kwa ajili ya uwekezaji)

Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini

109. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

- a) Utayarishaji wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti ya Uvuvi na mazao ya baharini;
- b) Kuandaa Mpango Mkakati wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na mazao ya baharini;
- c) Kuweka kumbukumbu ya tafiti zote zilizofanywa Zanzibar kuanzia mwaka 2000 kuhusiana na uvuvi na mazao ya baharini kwa ajili ya matumizi ya ndani na nje ya nchi;
- d) Kufanya utafiti wa uchumi jamii kwa wavuvi wa kienyeji;
- e) Kuanzisha maabara ya uvuvi na kuajiri wataalamu wa kutoa huduma bora za mazao ya baharini;
- f) Kuanzisha na kuendeleza mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kwa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na mazao ya baharini.

110. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka **wa** fedha 2019/2020, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini inaombewa jumla ya **TZS 250 milioni** ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini.

PROGRAMU KUU YA MIPANGO NA UTAWALA WA KAZI ZA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI

111. Mheshimiwa Spika, Programu ya Mipango na Utawala wa Kazi za Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi dhimumuni lake

kubwa ni kutoa huduma za kiofisi kwa ufanisi kwa ustawi wa sekta za kilimo.

Programu imegawika katika program ndogo tatu nazo ni:

- a) Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti;
- b) Programu ya Utawala na uendeshaji wa kazi za kilimo maliasili mifugo na uvuvi;
- c) Programu ndogo ya Uratibu wa Afisi Kuu Pemba.

112. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020, Programu ya Mipango na Utawala inaombewa jumla ya **TZS 17.73 bilioni** (TZS 5.29 bilioni ni mshahara, TZS 1.17 matumizi mengineyo, TZS 885.40 milioni ni kwa miradi ya maendeleo kutoka SMZ na TZS 10.38 bilioni kutoka kwa Washirika wa maendeleo).

Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti

113. Mheshimiwa Spika, Programu Ndogo ya Mipango Sera na Utafiti ina lengo la kuratibu kazi za mipango sera na utafiti kwa maendeleo ya sekta za kilimo, maliasili, mifugo na uvuvi. Programu ndogo hii itatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti 2019/2020

114. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Programu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

- a) Kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na maliasili;
- b) Kufanya tafiti tatu (2 Pemba na 1 Unguja) za kiuchumi na kijamii kuhusu mwenendo wa ushiriki wa vijana katika kilimo;
- c) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera na Programu za kupunguza umaskini katika kilimo na kuongeza kipato cha wakulima;
- d) Kufanya ziara za Ufutiliaji na tathmini za kazi za Wizara;
- e) Kushiriki katika mikutano sita (6) ya mashirikiano na Wizara za Sekta ya Kilimo Tanzania Bara, kikanda, kimataifa na Kitaifa;
- f) Kufanya mikutano minane (8) ya Kamati ya Utafiti;
- g) Kusimami utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Kilimo Zanzibar Z-ASDP;
- h) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Programu na Miradi iliyopo Wizarani.

115. Mheshimiwa Spika, programu ndogo ya Mipango inaombewa jumla ya **TZS 11.84 bilioni** (TZS 249.14 milioni mishahara, TZS 321.00 milioni kwa matumizi mengineyo, TZS

885.40 milioni kutoka SMZ kwa ajili ya Miradi ya maendeleo na TZS 10.38 kutoka kwa washirika wa maendeleo). Aidha, kwa mwaka 2019/20 programu itasimamia Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Masoko na Fedha Vijijini -MIVARF, Mradi wa Kuendeleza Uzalishaji wa Zao la Mpunga - ERPP, Mradi wa Kuwaunganisha Wakulima na Wazalishaji wa Mazao ya Mboga - Agri-Connect, Mradi wa Udhibiti wa Sumukuvu katika Mazao ya Nafaka- TANIPAC, Mradi wa Kukabiliana na Kilimo cha Mabadiliko ya Hali ya Hewa - Climate Smart Agriculture (Kiambatisho 8c; 8d; 8e).

Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji

116. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya utawala na uendeshaji ina lengo la kuimarisha mazingira bora **ya** utendaji kazi kwa ufanisi na maendeleo ya sekta za kilimo, misitu, mifugo na uvuvi.

Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji kwa Mwaka 2019/2020

- a) Kutoa maslahi kwa wafayakazi 1,200 na kuwawekea mazingira mazuri ya kazi;
- b) Kuwajengea uwezo wa kitaaluma Wafanyakazi 26 wanaoendelea na masomo 11 (1 PhD, 1 MSc, 8 Digirii na Diploma 1) Pamoja na wapya 15 (1PhD, 3 MSc, 5 Digirii, 3 Diploma na 3 Cheti);

- c) Udhhibit na ufuutiliaji wa mali za Serikali ikiwemo upimaji wa mashamba matatu (kilombero, Pangeni na Wesha) na kuyapatia hatimiliki;
- d) Kuendelea na ukaguzi wa mahesabu ya ndani pamoja na vikao vyta zabuni kwa ajili ya upatikanaji wa vifaa na huduma;
- e) Kuendelea na utoaji wa taarifa za sekta ya kilimo na maliasili kupitia vyombo vyta habari, majorida na kwa njia ya mtandao;
- f) Kufanya mafunzo kwa wastaaafu watarajiw.

117. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020, Programu ndogo ya utawala na mafunzo, inaombewa jumla ya **TZS 2.34 bilioni** kwa kazi za kawaida (TZS 1.84 bilioni ni mishahara na TZS 500.00 milioni kwa matumizi mengineyo).

Programu Ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba

118. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya uratibu wa Ofisi Kuu Pemba ina lengo la kuratibu maendeleo ya sekta ya kilimo, maliasili, mifugo na uvuvi. Programu ndogo hii inatoa huduma za utumishi za Wizara; kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi na kuratibu kazi za mipango ya Wizara ya Kilimo Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

119. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya uratibu wa Ofisi Kuu Pemba, kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020, Programu hii

inaombewa kutumia jumla ya **TZS 3.55 bilioni** (TZS 3.20 bilioni mishahara na TZS 350.00 milioni ni matumizi mengineyo).

MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

120. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inaomba kuidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS 88.17 bilioni** kati ya fedha hizo **TZS 22.98 bilioni** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS 11.42 bilioni Mishahara na TZS 5.70 bilioni matumizi mengineyo na TZS 5.86 bilioni RUZUKU kutoka SMZ kwa ajili ya Chuo cha Kilimo Kizimbani, Uvuvi, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar, Taasisi ya Utafiti wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo. Kwa kutekeleza programu na Miradi ya Maendeleo Wizara imetengewa **TZS 65.19 bilioni** (**TZS 60.26 bilioni** kutoka kwa washirika wa maendeleo na **TZS 4.93 bilioni** kutoka SMZ.

SHUKURANI

121. Mheshimiwa Spika, Baada ya uwasilishaji sasa natumia nafasi hii kuzishukuru na kuzipongeza nchi na Mashirika ya Kimataifa yaliyoisaidia Wizara katika juhudini za kuendeleza Kilimo, Mifugo na Uvuvi, zikiwemo Japan, China, India, Israel, Korea ya Kusini, Marekani, Misri, Oman na Uhlanzi, kwa kushirikiana na sisi kuendeleza sekta ya Kilimo nchini. Vilevile nayashukuru Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, ICRAF, IFAD, UNDP, FAO, JICA, UNICEF, WFP, USAID, USDA, KOICA, IITA, IRRI, CFC, AVRDC, AGRA, *Rockefeller Foundation* na *Bill and Melinda Gates Foundation*, GIZ, “WAP”, “WHO”, Shirika la Mionzi la Ulimwengu (IAEA), Indian Ocean Rim, Indian Ocean Tuna Commission (IOTC) na Umoja wa nchi za Ulaya - “EU” Vilevile, tunazishukuru taasisi za ndani kwa kuendeleza mashirikiano katika kutoa huduma za kilimo, maliasili, Mifugo na Uvuvi zikiwemo ZSTC, TAHA, UWAMWIMA, ZAIDI, COSTECH, Milele Foundation, Kilimo Trust, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi Tanzania Bara, CARI, Wizara ya Maliasili na Wizara ya Ushirikiano ya Afrika Mashariki, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu ya Tanzania, Taasisi ya Sayansi ya Baharini, “State Oceanic Administration” (SOA) ya China, Heifer Project Tanzania, Zanchick, “ZAASO”, “ZSPCA” na “WIOMSA”

122. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za pekee, kwa wakulima, Wafugaji, Wavuvi na Wanakamati za hifadhi za Maliasili kwa kazi kubwa wanayoifanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, mifugo na mazao ya Baharini. Pia Napenda kumshukuru Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Manaibu wake wawili wa Wizara ya Kilimo, Afisa Mdhamsini WKMMU pamoja na Wakurugenzi wa Idara, Taasisi na Asasi zote za Wizara hii; watumishi wote wa Wizara pasi na kuwasahau wadau wote wa Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa juhud, ushirikiano na ushauri uliowezesha kutekelezwa kwa Shabaha za Wizara kwa mwaka 2018/2019. Ni matarajio kwamba tutaendelea kushirikiana tena katika mwaka 2019/2020.


123. Mheshimiwa Spika, Napenda kuwashukuru Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Madiwani, Masheha, Kamati za Maendeleo za Shehia, Kamati za Wakulima, Wafugaji na Wavuvi, Vikosi vya SMZ na vyombo vya habari kwa mashirikiano yao mazuri waliyoyatoa kusaidia utekelezaji wa kazi zetu, Mwisho natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kufanikisha kuchapishwa kwa hotuba hii ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

124. Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni kwa kunisikiliza na naomba kutoa hoja.


**MHE. MMANGA MJENGO MJAWIRI (MBM)
WAZIRI, WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO
NA UVUVI - ZANZIBAR**

VIAMBATISHO


Kiambatisho Nam.1a




Kiambatisho Nam.1b



Kiambatisho Nam. 1c



Kiambatisho Nam.1d



Kiambatisho Nam.2

Jaduweli la Upatikanaji wa Mapato Julai 2018 hadi Aprili 2019

IDARA	MAELEZO	BAJETI (TZS) 2018/2019			UKUSANYAJI HALISI (TZS) 2018/2019		
		PEMBA	UNGUJA	JUMLA	PEMBA	UNGUJA	JUMLA
IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZO REJESHEKA							
1422022	ADA YA MAZAO YA MISITU	60,000,000	278,400,000	338,400,000	24,574,500	282,706,585	307,281,085
1422023	ADA YA UUZAJI WA MAWE NA MICHANGA NA KOKOTO	650,000,000	7,775,600,000	8,425,600,000	359,097,870	4,628,794,730	4,987,892,600
1421001	MAUZO YA UZALISHAJI WA MICHE	35,000,000	15,000,000	50,000,000	492,000	1,358,000	1,850,000
JUMLA YA IDARA		745,000,000	8,089,000,000	8,814,000,000	384,164,370	4,912,859,315	5,297,023,685
IDARA YA KILIMO							
1422048	ADA UKAGUZI WA MAZAO	15,000,000	75,000,000	90,000,000	15,171,500	56,729,160	71,900,660
JUMLA YA IDARA		15,000,000	75,000,000	90,000,000	15,171,500	56,729,160	71,900,660
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO							
1423002	MAUZAJI YA MAZAO NA MICHE	5,000,000	70,000,000	75,000,000	-	7,884,600	7,884,600
1422060	MAPATO YA	224,000,000	20,000,000	244,000,000	300,000	22,260,000	22,560,000

IDARA	MAELEZO	BAJETI (TZS) 2018/2019			UKUSANYAJI HALISI (TZS) 2018/2019		
		PEMBA	UNGUJA	JUMLA	PEMBA	UNGUJA	JUMLA
	MASHAMBA						
1422066	ADA YA UINGIZAJI WAGENI	9,000,000	50,000,000	59,000,000	5,803,500	9,777,000	15,580,500
	JUMLA YA IDARA	238,000,000	140,000,000	378,000,000	6,103,500	39,921,600	46,025,100
IDARA YA UVUVI							
1422026	LESENI ZA UVUVI	18,000,000	280,000,000	298,000,000	23,472,500	48,378,610	71,851,110
1422067	MAPATO YA UVUVI WA BAHARI KUU	-	2,320,000,000	2,320,000,000		-	-
1422027	ADAYA KIBALI CHA USA FIRISHAJI MAZAO BAHARINI	10,000,000	450,000,000	460,000,000	8,801,700	272,978,527	281,780,227
	JUMLA YA IDARA	28,000,000	3,050,000,000	3,078,000,000	32,274,200	321,357,137	353,631,337
IDARA YA MIFUGO							
1421011	UTIBABU WA WANYAMA	15,000,000	20,000,000	35,000,000	11,905,250	68,929,300	80,834,550
1422068	MAPATO YA MIFUGO	35,000,000	70,000,000	105,000,000	455,300	1,071,000	1,526,300
	JUMLA YA IDARA	50,000,000	90,000,000	140,000,000	12,360,550	70,000,300	82,360,850
JUMLA YA WIZARA		1,146,000,000	11,354,000,000	12,500,000,000	449,868,620	5,406,284,512	5,856,153,132

Kiambatisho Nam.3

UPATIKANAJI WA FEDHA ZA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA JULAI 2018 - APRILI 2019

Program Kuu/Program Ndogo	Fedha Iliyopatikana Kwa Kipindi Cha Julai-Aprili 2019						
	Mshahara	Matumizi Kawaida	Ruzuku Kawaida	Ruzuku Mshahara	Maendeleo Smz	Maendeleo Mhisani	Jumla
PL0101 Maendeleo ya Kilimo	3 ,775,250,649	3,172,360,000	836,761,126	1,176,368,787	5 00,000,000	42,263,000,000	51,723,740,562
SL010101 Umwagiliaji maji	577,968,440	368,900,000			500,000,000	42,263,000,000	43,709,868,440
SL010102 Utafiti na Mafunzo ya kilimo	1,555,653,955	268,460,000	112,833,750	652,252,814			2,589,200,519
SL010103 Maendeleo ya huduma za kilimo	1,453,301,685	1,985,000,000					3,438,301,685
SL010104 Uhakika wa chakula na lishe	188,326,569	550,000,000					738,326,569
SL010105 Karakana ya Matrekta	-	-	723,927,376	524,115,973			1,248,043,349
PL0102 Maendeleo ya Rasilimali za Misitu na Maliasili Zisizorejesheka	1,578,212,780	421,708,015	-	-	-	-	1,999,920,795

Program Kuu/Program Ndogo	Fedha Iliyopatikana Kwa Kipindi Cha Julai-Aprili 2019						
	Mshahara	Matumizi Kawaida	Ruzuku Kawaida	Ruzuku Mshahara	Maendeleo Smz	Maendeleo Mhisani	Jumla
SL010201 Uhifadhi wa misitu		186,935,158					186,935,158
SL010202 Maendeleo ya misitu	1,578,212,780	234,772,857					1,812,985,637
PL0103 Maendeleo ya Mifugo	1,296,232,650	290,600,000	377,238,192	202,451,405	603,200,000	-	2,769,722,247
SL010301 Uzalishaji wa mifugo	-	175,000,000			603,200,000		778,200,000
SL010302 Huduma za utabibu wa mifugo	1,296,232,650	115,600,000					1,411,832,650
SL010303 Taasisi ya Utafiti wa mifugo			377,238,192	202,451,405			579,689,597
PL0104 Maendeleo ya Uvubi	681,864,730	375,000,000	-	-	-	1,439,753,675	2,496,618,405
SL010401 K. ufgajji wa mazao ya baharini		225,000,000					225,000,000
SL010402 Maendeleo ya uvubi na hifadhi	681,864,730	150,000,000				1,439,753,675	2,271,618,405

Program Kuu/Program Ndogo	Fedha Iliyopatikana Kwa Kipindi Cha Julai-Aprili 2019						
	Mshahara	Matumizi Kawaida	Ruzuku Kawaida	Ruzuku Mshahara	Maendeleo Smz	Maendeleo Mhisani	Jumla
baharini							
PL0105 Mipango na Usimamizi wa Kilimo, Maliasili, Mifugo, na Uvuvu	4,333,309,551	1,137,983,200	-	-	380,000,000	,362,437,661	8,213,730,412
SL010501 Utawala na uendeshaji wa kazi za kilimo maliasili mifugo na uvuvu	1,346,138,836	685,000,000					2,031,138,836
SL010502 Mipango, sera na utafiti wa kilimo maliasili mifugo na uvuvu	251,387,970	395,000,000			380,000,000	,362,437,661	3,388,825,631
SL010503 Uratibu Ofisi kuu Pemba	2,735,782,745	57,983,200					2,793,765,945
Jumla Kuu	11,664,870,360	5,397,651,216	1,213,999,318	1,378,820,192	1 ,483,200,000	6,065,191,336	67,203,732,422

Kiambatisho Nam.4

Jaduweli la Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo Julai 2018 hadi Aprili 2019

MRADI	MAKISIO 2018/2019			FEDHA ZILOPATIKANA		
	SMZ	MUHISANI	JUMLA	SMZ	MUHISANI	JUMLA
Mradi wa umwagiliaji maji -KOREA	500,000,000	8,500,000,000	9,000,000,000	500,000,000	42,263,000,000	42,763,000,000
Mradi wa Miundombinu ya mifugo-SMZ	856,000,000	-	856,000,000	603,200,000	-	603,200,000
Mradi wa Uimarishaji mazao ya baharini – FAO	200,000,000	6,700,000,000	6,900,000,000			
Mradi wa Usimamizi Uvuvu Bahari Kuu - SWIOFish	50,000,000	2,152,220,000	2,202,220,000	-	1,439,753,675	1,439,753,675
Ujenzi wa Soko la Malindi	3,666,000,000	6,750,000,000	10,416,000,000			
MIVARF	300,000,000	950,000,000	1,250,000,000	300,000,000	695,419,800	995,419,800

MRADI	MAKISIO 2018/2019			FEDHA ZILOPATIKANA		
	SMZ	MUHISANI	JUMLA	SMZ	MUHISANI	JUMLA
ERPP	80,000,000	4,735,700,000	4,815,700,000	80,000,000	1,667,017,861	1,747,017,861
Safeguarding Zanzibar Forest And Coastal Habitats For Multiple Ben		223,220,000	223,220,000			
Food Climate Resilient Project		71,860,000	71,860,000			
Tanzania Initiative For Preventing Aflatoxin Contamination (Tanipac)		1,890,000,000	1,890,000,000			
Agri-Connect- Supporting Value Chains For Shared Prosperity		1,760,000,000	1,760,000,000			
Jumla	5,652,000,000	33,733,000,000	39,385,000,000	1,483,200,000	46,065,191,336	47,548,391,136

Kiambatisho Nam.5

Jaduweli la Makadirio ya Ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa Fedha 2019/20

IDARA	MAELEZO	PEMBA	UNGUJA	JUMLA
IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZO REJESHEKA				
1422022	ADA YA MAZAO YA MISITU	79,000,000	207,129,600	286,129,600
1422023	ADA YA MCHANGA, KIFUSI NA MAWE	788,448,000	6,904,076,000	7,692,524,000
1421001	MAUZO YA UZALISHAJI WA MICHE	38,500,000	11,160,000	49,660,000
	JUMLA YA IDARA	905,948,000	7,122,365,600	8,028,313,600
IDARA YA KILIMO				
1422048	ADA UKAGUZI WA MAZAO	22,800,000	55,800,000	78,600,000
	JUMLA YA IDARA	22,800,000	55,800,000	78,600,000
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO				
1423002	MAUZAJI YA MAZAO NA MICHE	-	52,080,000	52,080,000
1422060	MAPATO YA MASHAMBA	206,000,000	14,880,000	220,880,000
1422066	ADA YA UINGIZAJI WAGENI	13,000,000	37,200,000	50,200,000
	JUMLA YA IDARA	219,000,000	104,160,000	323,160,000
IDARA YA UVUVI				
1422026	LESENI ZA UVUVI	21,900,000	116,250,000	138,150,000
1422067	MAPATO YA UVUVI WA BAHARI KUU	-	1,526,080,000	1526080000
1422027	ADA YA USAFIRISHAJI MAZAO YA BAHARINI	12,377,000	234,800,000	247,177,000
	JUMLA YA IDARA	34,277,000	1,877,130,000	1,911,407,000
IDARA YA MIFUGO				
1421011	UTIBABU WA WANYAMA	42,500,000	52,080,000	94,580,000
1422068	MAPATO YA MIFUGO	18,000,000	14,203,000	32,203,000
	JUMLA YA IDARA	60,500,000	66,283,000	126,783,000
	JUMLA YA WIZARA	1,243,525,000	9,225,738,600	10,468,263,600

Kiambatanisho Nam. 6 Jadueli la makadirio ya Fedha za Kazi za Kawaida kwa mwaka 2019/20

PROGRAM KUU/PROGRAM NDOGO	MAKADIRIO						
	MSAHARA	MATUMIZI KAWAIDA	RUZUKU KAWAIDA	RUZUKU MSAHARA	SMZ	MHISANI	JUMLA
PL0101 Maendeleo ya Kilimo	2,383,517,733	3,501,000,000	1,523,700,000	3,229,000,000	1,000,000,000	32,867,000,000	44,504,217,733
SL010101 Umwagiliaji maji	560,071,000	300,000,000			1,000,000,000	32,867,000,000	34,727,071,000
SL010102 Utafiti na Mafunzo ya kilimo			722,800,000	2,614,200,000			3,337,000,000
SL010103 Maendeleo ya huduma za kilimo	1,602,089,000	2,701,000,000					4,303,089,000
SL010104 Uhakika wa chakula na lishe	221,357,733	500,000,000					721,357,733
SL010105 Karakana ya Matreksa	-	-	800,900,000	614,800,000			1,415,700,000
PL0102 Maendeleo ya Rasilimali za	1,674,317,736	391,880,000	-	-	-	228,200,000	2,294,397,736

PROGRAM KUU/PROGRAM NDOGO	MAKADIRIO						
	MSAHARA	MATUMIZI KAWAIDA	RUZUKU KAWAIDA	RUZUKU MSAHARA	SMZ	MHISANI	JUMLA
Misitu na Maliasili Zisizorejesheka							
SL010201 Uhifadhi wa misitu		114,605,000				228,200,000	342,805,000
SL010202 Maendeleo ya misitu	1,674,317,736	277,275,000					1,951,592,736
PL0103 Maendeleo ya Mifugo	1,303,490,305	254,812,000	556,500,000	305,700,000	1,394,595,000	-	3,815,097,305
SL010301 Uzalishaji wa mifugo		108,966,000			194,595,000		303,561,000
SL010302 Huduma za utabibu wa mifugo	1,303,490,305	145,846,000					1,449,336,305
SL010303 Taasisi ya Utafiti wa mifugo	-		556,500,000	305,700,000	1,200,000,000		2,062,200,000
PL0104 Maendeleo ya Uvusi	763,785,682	378,208,000	250,000,000	-	1,650,000,000	16,786,801,000	19,828,794,682
SL010401 Kuimarisha ufugaji wa mazao ya baharini		178,208,000					178,208,000

PROGRAM KUU/PROGRAM NDOGO	MAKADIRIO						
	MSAHARA	MATUMIZI KAWAIDA	RUZUKU KAWAIDA	RUZUKU MSAHARA	SMZ	MHISANI	JUMLA
SL010402 Maendeleo ya uvuvi na hifadhi za baharini	763,785,682	200,000,000	250,000,000		1,650,000,000	16,786,801,000	19,650,586,682
PL0105 Mipango na Usimamizi wa Kilimo, Maliasili, Mifugo, na Uvuvu	5,291,688,205	1,171,000,000	-	-	885,405,000	10,382,699,000	17,730,792,205
SL010501 Utawala na uendeshaji wa kazi za kilimo maliasili mifugo na uvuvi	1,839,225,000	500,000,000					2,339,225,000
SL010502 Mipango, sera na utafiti wa kilimo maliasili mifugo na uvuvi	249,149,205	321,000,000			885,405,000	10,382,699,000	11,838,253,205
SL010503 Uratibu Ofisi kuu Pemba	3,203,314,000	350,000,000					3,553,314,000
Jumla Kuu	11,416,799,661	5,696,900,000	2,330,200,000	3,534,700,000	4,930,000,000	60,264,700,000	88,173,299,661

Kiambatisho Nam.7: Jaduweli la Makadirio ya Fedha za Maendeleo kwa mwaka 2019/2020

MRADI	MHISANI	MAKADIRIO			
		SMZ	MUHISANI		JUMLA
			MKOPO	RUZUKU	
UIMARISHAJI WA MIUNDOMBINU YA U/MAJI	KOREA	1,000,000,000	32,867,000,000	-	33,867,000,000
MRADI WA MIUNDOMBINU YA SEKTA YA KILIMO	SMZ	1,000,000,000	-	-	1,000,000,000
PROGRAMU YA KUENDELEZA UTAFITI WA MIFUGO	SMZ	1,200,000,000			1,200,000,000
MRADI WA KUIMARISHA UFUGAJI WA MAZAO YA BAHARINI – <i>Hatchery</i>	FAO	200,000,000	-	692,423,000	892,423,000
USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA UVUVI – <i>SWIfish</i>	W/BANK	50,000,000	2,894,693,000	-	2,944,693,000
UJENZI WA SOKO LA MALINDI	JICA	1,400,000,000	0	13,200,000,000	14,600,000,000
UEENDELEZAJI WA MIUNDOMBINU YA SOKO, KUONGEZA THAMANI NA	ADB,IFAD		399,616,000	-	399,616,000

MRADI	MHISANI	MAKADIRIO			
		SMZ	MUHISANI		JUMLA
			MKOPO	RUZUKU	
MISAADA VIJJINI-MIVARF					
UPANUZI WA UZALISHAJI WA MCHELE – ERPP	W/BANK	80,000,000	-	6,950,283,000	7,030,283000
SAFEGUARDING ZANZIBAR FOREST AND COASTAL HABITATS FOR MULTIPLE BENEFICIARY	UNDP	-	-	228,200,000	228,200,000
FOOD CLIMATE RESILIENT PROJECT	USDA USAID	-	-	44,400,000	44,400,000
TANZANIA INITIATIVE FOR PREVENTING AFLATOXIN CONTAMINATION (TANIPAC)	AFDB	-	-	988,440,000	988,440,000
AGRI-CONNECT- SUPPORTING VALUE CHAINS FOR SHARED PROSPERITY	EDF-EU	-	-	2,000,000,000	2,000,000,000
JUMLA		4,930,000,000	36,161,309,000	24,103,746,000	65,195,055,000

Kiambatisho Nam.8a:

MRADI WA USIMAMIZI WA KAZI ZA UVUVI WA KANDA YA KUSINI MASHARIKI MWA BAHARI YA HINDI (SWIOFish)

Gharama za mradi: **Kwa mwaka 2018/2019** Mradi uliombewa **TZS. 50,000,000** kutoka SMZ na **TZS. 2,152,220,000**. Hadi kufikia Aprili, 2018 mradi ulipatiwa **TZS. 1,439,753,675** kutoka kwa washirika wa maendeleo na hakuna fedha zilizopatikana kutoka SMZ.

Lengo Kuu la mradi: ni kuimarisha usimamaizi wa shughuli za uvuvi.

Malengo ya mwaka 2018/2019

Kuimarisha usimamizi wa uvuvi maalumu (uliopewa kipaumbele).

Kuongeza kipato kutokana na shughuli za uvuvi maalum wa kanda.

Uratibu na Usimamizi wa Mradi wa SWIOFish.

Utekelezaji wa Malengo

Wataalamu wa Uvuvi watano (5) pamoja na wanajamii wane (4) wametembelea Madagascar kujifunza uzoefu wa Ufungaji pweza;

Mikutano ya vijiji na kamati tendaji za maeneo ya hifadhi zimeendelea kufanyika;

Kupatikana kwa maandiko ya mradi kwa tafiti tatu za Jodari mbili na uvuvi wa miambani pamoja na kupatikana kwa hadudi tejea kwa utayarishaji wa andiko kwa uvuvi wa samaki jamii ya dagaa na pweza;

Kuanzishwa kwa mfumo wa ukusanyaji na uhifadhi wa takwimu za uvuvi na mtandao wake kwa ajili ya wananchi kujipatia

taarifa za uvuvi kwa muda husika (SAMAKI Information System);

Kupatikana kwa mpango mkuu wa miaka 15 wa Usimamizi na Uendelezaji wa Uvuvi (Zanzibar Fisheries Masterplan);

Kuongezeka kwa ukataji wa leseni za Uvuvi na vyombo vya uvuvi kutoka asilimia 15% mwaka 2016/2017 hadi asilimia 35% mpaka sasa;

Kupatikana kwa Mkakati wa mawasiliano (CARS) kwa ajili ya kusambasa taarifa za mradi kwa jamii kuitia njia mbali mbali za mawasiliano ikiwemo vyombo vya habari;

Kupatikana kwa rasimu ya mwisho ya mchoro kwa ajili ya ujenzi wa Afisi za maeneo ya Hifadhi ya Mkokotoni na Maeneo ya Hifadhi ya Visiwa vya Changuu na Bawe pamoja na kituo cha doria kisiwani Pungume.

Gharama kwa mwaka 2019/2020. Mradi unaombewa TZS. 50,000,000 kutoka SMZ na TZS. 2,894,693 kutoka kwa washirika wa maendeleo (Benki ya Dunia)

Malengo kwa mwaka 2019/2020

Kuboresha usimamizi wa uvuvi maalumu (uliopewa kipaumbele).

Kuongeza kipato kutokana na shughuli za uvuvi maalum wa kanda.

Uratibu na Usimamizi wa Mradi wa SWIOFish.

Ujenzi wa Maabara na Ofisi ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi

Ujenzi wa Chelezo katika eneo la Kampuni ya uvuvi

Kuendeleza mafunzo kwa wanafunzi 13 (3 Uzamivu 10 Uzamili)

Kukamilisha mpango wa usimamizi na uendeshaji wa maeneo ya uhifadhi (MIMCA, MENAI, PECCA, CHABAMCA)

Kiambatisho Nam.8b**MRADI WA KUIMARISHA UFUGAJI WA MAZAO YA BAHARINI**

JINA LA MRADI	MRADI WA KUIMARISHA UFUGAJI WA MAZAO YA BAHARINI
MUDA WA MRADI	2012/2013 – 2019/2020
JUMLA YA GHARAMA	Gharama za mradi huu hupangwa kila mwaka na kuidhinishwa na mfadhili na Serikali
LENGO KUU	Kuimarisha ufugaji wa samaki na mazao mengine ya baharini
FEDHA ZILIZOTENGWA 2018/2019	Jumla ya shilingi 200,000,000 kutoka Serikalini (SMZ) na shilingi 6,700,000,000 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo (FAO) zilitengwa kutekeleza Mradi huu kwa mwaka wa fedha 2018/2019.
Malengo ya Mwaka wa fedha 2018/2019: Kufanya ujenzi wa kituo cha uzalishaji wa vifaranga (hatchery), vya samaki, kaa na majongoo bahari; na Kujenga uwezo kwa wafanyakazi katika kuendeleza ufugaji wa mazao ya baharini na uendeshaji wa “hatchery”.	
Utekelezaji mwaka 2018/2019: Ujenzi wa kituo cha uzalishaji wa vifaranga (hatchery), vya samaki, kaa na majongoo bahari umekamilika; Wafugaji wa samaki 22 wamepatiwa mafunzo bora ya ufugaji wa samaki.	

Gharama za Mradi kwa mwaka 2019/2020

Jumla ya TZS. 200,000,000 kutoka SMZ na TZS.692,423,000 kutoka FAO zimetengwa kutekeleza mradi huu kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Malengo ya mwaka wa fedha 2019/2020:

Kuzalisha vifaranga nya samaki milioni 10, kaa na majongoo bahari;

Kujenga uwezo kwa wafugaji wa samaki na wafanyakazi katika kuendeleza ufugaji bora wa mazao ya baharini na uendeshaji wa “hatchery”;

Kuanzisha kituo cha kupokea vifaranga nya samaki, kaa na majongoo bahari Pemba.

Kiambatisho Nam.8c**PROGRAMU YA MIUNDOMBINU YA MASOKO, UONGEZAJI THAMANI MAZAO NA HUDUMA ZA KIFEDHA VIJIJINI - MIVARF**

NAM	SHUGHULI	UTEKELEZAJI
	Kwa mwaka wa fedha 2018/2019, jumla ya shilingi 300,000,000 kutoka Serikalini (SMZ) na shilingi 950,000,000 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo	
1.	Kusaidia na kuendelea kujenga uwezo wa Mabaraza ya Wakulima;	Mabaraza ya Wakulima katika wilaya 10 yamewezeshwa kuendesha kazi zao, ikiwemo mikutano, pamoja na nyenzo za kuendesha ofisi (stationery na mawasiliano), pamoja na ukarabati wa ofisi.
2.	Kuwezesha kufanyika kwa mikutano ya robo mwaka ya Kamati za Wilaya na Mabaraza ya wakulima;	Mikutano ya robo mwaka imefanyika na kujimuisha wajumbe wa mabaraza ya wakulima na kamati za usimamizi za Wilaya
3.	Kuwawezesha wazalishaji na kuwaunganisha na masoko kupitia Washauri Elekezi (Business Coaches kwa mazao ya mihogo, ndizi, mpunga mboga/matunda) na samaki	Baada ya kusainiwa mikataba, washauri elekezi wanne (4) katika masuala ya (i) fedha vijijini; (ii) uongezaji thamani mazao ya mboga na matunda; (iii) uongezaji thamani dagaa; pamoja na (iv) kuunganisha wazalishaji na masoko wametekeliza kazi zao.

4.	<p>Kuwawezesha wazalishaji kufikia na kupata mikopo kutoka kwa Taasisi za Fedha chini ya muongozo na usimamizi wa Mshauri Elekezi wa Huduma ndogo ndogo za kifedha;</p>	<p>Jumla yay a SACCOS 20 na Vikundi vya wazalishaji 50 vimenufaika na huduma za mshauri elekezi. Kazi zilizofanyika ni pamoja na :</p> <ul style="list-style-type: none"> i. Kutathmini uwezo wa uendeshaji, mahitaji ya fedha na vigezo vya kukopesheka katika vikundi vya uzalishaji na SACCOS ii. Mapitio na marekebisho ya katiba na sheria ndogondogo za vikundi na SACCOS ili kuwawezesha kukubalika na taasisi za kifedha iii. Miongozo ifuatayo (operational guidelines) imepitiwa, kuboreshwa na kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili: (i) upatikanaji fedha kupitia ‘Mfuko wa ubunifu (Rural Innovation Fund)’ na ; (ii) Jinsi ya kuandaa katiba bora za SACCOS (iii) Muongozo wa kuweka na kukopa kwa ajili ya SACCOS iv. Utunzaji wa mali na dhima katika SACCOS v. Utayarishaji wa katiba za SACCOS vi. Vikao vya pamoja baina ya walengwa kupitia vikundi vya wazalishaji na SACCOS na AMCOS, na wawakilishi wa taasisi za fedha na benki za CRDB, Postal Bank nk vii. Kutayarisha mipango ya biashara (Business Plans) kwa
----	---	--

		vikundi na SACCOS/ viii. Mafunzo juu ya udhibiti wa mikopo na utunzaji wa kumbukumbu za kifendha yametolewa kwa vikundi ambapo wawakilishi watatu kwa kila kikundi wameshiriki.
5.	Kuwezesha wazalishaji kushiriki maonesho ya kilimo	Jumla ya wawakilishi wa vikundi 30 kutoka Unguja na Pemba waliwezeshwaa kushiriki katika maonesha ya nane nane yaliyofanyika katika viwanja vya Dole Unguja na siku ya chakula duniani yaliyofanyika Chamanangwe Pemba.
6.	Kuwezesha ziara ya mafunzo kwa wawakilishi wa vikundi vya wakulima na wasarifu wa mazao;	Ziara hazijafanyika, aidha zinatarajiwa kufanyika katika robo ya tatu ya utekelezaji. Ziara hizi hufanyika baada ya kumaliza mafunzo ya nadharia.
7.	Kushirikiana na Wizara ya Fedha kukamilisha Sera, Mkakati wa Utekelezaji na Sheria ya Huduma Ndogo Ndogo za Kifedha;	Programu imeendesha warsha ya wadau kwa ajili ya ukamilishaji Sera, na Mkakati wa Utekelezaji na Sheria ya Huduma Ndogo Ndogo za Kifedha. Warsha hii ilihudhuriwa na wadau wakiwemo wazalishaji na wasindikaji wa mazao ya kilimo, NGOs, taasisi za fedha na benki za biashara na Benki Kuu ya Tanzania.

8.	Uendeshaji na usimamizi wa Programu	Programu imewawezesha maofisa wa Wilaya 11 na Mikoa yote mitano ya Zanzibar kufanya usimamizi ufuatiliaji wa kazi mbali mbali, kwa usafiri pamoja na vikao vya utekelezaji na kutoa ripoti kama zinavyotakiwa.
kwa mwaka wa fedha 2019/2020., jumla ya shilingi 399,616,000 kutoka kwa washirika wa maendeleo		
<p>Kusaidia na kuendelea kujenga uwezo wa Mabaraza ya Wakulima;</p> <p>Kuwezesha kufanyika kwa mikutano ya robo mwaka ya Kamati za Wilaya na Mabaraza ya wakulima;</p> <p>Kuwawezesha wazalishaji na kuwaunganisha na masoko kuptitia Washauri Elekezi (Business Coaches kwa mazao ya mihogo, ndizi, mpunga mboga/matunda) na samaki</p> <p>Kuwawezesha wazalishaji kufikia na kupata mikopo kutoka kwa Taasisi za Fedha chini ya muongozo na usimamizi wa Mshauri Elekezi wa Huduma ndogo ndogo za kifedha;</p>		

Kiambatisho Nam.8d

MRADI WA KUIMARISHA UZALISHAJI WA MPUNGA (ERPP)

Gharama za mradi kwa mwaka 2018/2019: Kwa mwaka 2018/2019 Mradi uliombewa TZS. 4,735,700,000 kutoka Benki ya Dunia na TZS. 80,000,000 kutoka Serikalini. Hadi kufikia Aprli, 2018 fedha zilizopatikana kutoka Benki ya Dunia ni TZS 1,667,017,861 na TZS 80,000,000 kutoka serikalini.	
Malengo ya Mwaka 2018/2019	Utekelezaji wa Malengo
Kuzalisha mbegu bora za mpunga kilo 400 za daraja la msingi na tani 15 za mbegu za mpunga (SARO 5 na SUPA BC) zilizothibitishwa (Certified seeds grade);	Jumla ya kilo 400 za mbegu daraja la msingi na tani 12.1 za mbegu daraja la ‘certified’ zimezalishwa.
Kufanya ziara mbili (2) za siku ya wakulima shambani Unguja na Pemba;	Wakulima 260 wameshiriki katika ziara 2 za Siku ya Wakulima Shambani (Farmers’ Field Day).
Kutoa mafunzo ya udhibiti wa ubora wa viwango vya mbegu kwa wakaguzi wa mashamba ya mbegu wanane (8) na wataalamu wa maabara wanne (4);	Mafunzo yametolewa na TOSCI kwa Wakaguzi wa mbegu wanane (8) na Wataalamu wa maabara wanne (4).
Kutoa mafunzo ya matumizi ya vifaa vya kisasa vya upimaji ardhi kwa wataalamu wa umwagiliaji 14 pamoja na softwares’ za uandaaji wa michoro na ramani kwa	Mafunzo ya uandaaji wa ramani na michoro kwa kutumia “design software” yametolewa kwa wahandisi wa umwagiliaji 10 (wanaume 7 na

wahandisi wa umwagiliaji saba (7) Unguja na Pemba;	wanawake watatu).
Kuandaa ziara za mafunzo kwa Jumuiya za Umwagiliaji kutoka skimu 16 Unguja na Pemba;	Jumla ya wakulima 16 (wanaume 9 na wanawake 7) wameshiriki ziara za mafunzo katika Chuo cha Kilimo cha Kilimanjaro (KATC), skimu za umwagiliaji za Lower Moshi na Leki Tatu.
Kujenga/kukarabati miundombinu katika skimu tisa (9) za umwagiliaji maji;	<ul style="list-style-type: none"> ● Visima 6 vya umwagiliji vimechimbwa katika skimu za Kibondemzungu, Koani, Bandamaji, Machigini, Dobi na Ole ● Kazi za uungaji umeme zimefanyika mabonde ya Kibondemzungu, Koani, Mchangani, Bandamaji, Machigini, Dobi na Ole ● Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu za Mtwango na Kwalempona unaendelea; Mtwango ujenzi umefikia asilimia 65 na Kwalempona asilimia 45. ● Upitiaji wa michoro na ramani pamoja na utayarishaji wa Kabrasha la Zabuni kwa skimu 7 (Kibondemzungu, Koani, Mchangani, Bandamaji, Machigini, Dobi na Ole) umefanyika kupitia Mshauri Mwelekezi,

	Kampuni ya NORPLAN umefanyika.
Kuanzisha mashamba ya maonesho 200 ya Kilimo Shadidi cha Mpunga (130 Unguja na 70 Pemba);	Jumla ya mashamba 25 (15 Unguja na 10 Pemba) ya maonesho yameanzishwa.
Kutoa mafunzo ya Kilimo Shadidi cha Mpunga kwa wakulima 1,500 wa Unguja na Pemba;	Mafunzo ya Kilimo Shadidi cha Mpunga yametolewa kwa wakulima 750 (450 Unguja na 300 Pemba).
Kutoa Ruzuku ya Pembejeo za mpunga kwa wakulima katika maeneo ya umwagiliaji, Unguja na Pemba;	Jumla ya tani za mbolea (UREA tani 53,9, DAP tani 4 na TSP tani 8) zimesambazwa katika skimu za umwagiliaji zilizo chini ya Mpango wa Ruzuku wa Mradi wa ERPP.
Kutoa mafunzo kwa Maafisa ugani 40 (wanaume 20 na wanawake 20) wa maeneo ya Umwagiliaji, Unguja na Pemba.	Mafunzo ya mbinu bora za uzalishaji wa mpunga yametolewa kwa Maafisa Ugani 40 (20 wanaume na 20 wanawake).

Kiambatisho Nam.8e MRADI WA UENDELEZAJI MIUNDOMBINU YA MIFUGO

Gharama za mradi: Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Mradi huu ulipangwiwa TZS. 856,000,000 kutoka SMZ. Hadi kufikia Aprili, 2018 mradi umepata TZS. 603,200,000 kutoka SMZ.

Lengo Kuu la mradi: Kuimarisha miundombinu ya mifugo ya uzalishaji na masoko ili kuongeza uzalishaji na thamani ya mazao yatokanayo na mifugo na bidhaa za mifugo.

Malengo ya mwaka 2018/2019

Kufanya ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za utibabu, uzalishaji na mafunzo ya mifugo (Fuoni-Unguja, kituo cha mifugo Ole na Magome –Pemba;

Kuanzisha kituo cha Karantini ya mifugo huko Gando, Pemba;

Kuimarisha shamba la Mifugo-Pangeni kwa kuchimba kisima;

Kufanya “survey” ya mifugo

Utekelezaji wa Malengo

Ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za utabibu na uzalishaji mifugo umekamilika.

Kazi ya uchimbaji wa visima viwili na ujenzi wa minara shamba la mifugo Pangeni umekamilika.

Ulipaji wa fidia na ujenzi wa jengo la ofisi umekamilika na mkataba wa ujenzi wa uzio wa Karantini shamba la Gando umesainiwa na Kampuni ya MASIM.

“Survey” ya Mifugo inaendelea kufanyika

Gharama kwa mwaka 2019/2020: Mradi unaombewa TZS. 1,000,000,000 kutoka SMZ

Malengo kwa mwaka 2019/2020

Kuimarisha vituo vya karanti ya mifugo vya Gando na Donge Muwanda kwa kujenga josho,

Kukarabati Ghala la akiba ya chakula la Pemba na maghala ya kuhifadhi pembejeo ya kilimo, maabara ya utafiti Kizimbani na Nyumba za Wafanyakazi;

Kuendeleza wafugaji wadogo wadogo.

Makadirio ya Fedha za kazi za Kawaida kwa Mwaka 2019/20

